

**ATHARI YA KISWAHILI SANIFU KATIKA MSAMIATI WA LAHAJA YA  
KIMAKUNDUCHI**

**ZUBEIDA MOH'D CHUM**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA  
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADAYA UZAMILI  
(M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

**ITHIBATI**

Aliyesaini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii inayoitwa “**Athari ya Kiswahili Sanifu Katika Msamiati wa Lahaja Ya Kimakunduchi**” na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa shahada ya uzamili (M.A. Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

---

**Dkt. Zelda Elisifa**

**(Msimamizi)**

Tarehe.....

## **HAKIMILIKI**

Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au/na kutoa kivuli japo sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**TAMKO**

Mimi, Zubeida Moh'd Chum, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya utunuku wa shahada yoyote.

.....

Sahihi

.....

Tarehe

**TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa, Bi Fatma Mwinyi na Bw. Moh'd Chum. Juhudi zao za kunilea na kunisomesha tokea hatua za awali ndio zilizonifanya niwe hapa nilipo.

## **SHUKURANI**

Kwanza kabisa namshukuru Allah (S.W), Muumba wa mbingu, ardhi na kila kilichopo katika ulimwengu. Yeye ndiye aliyenipa afya, uzima, maarifa na uwezo wa ufahamu wa kufanya utafiti huu. Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Dkt. Zelda Elisifa, kwa muongozo, ushauri na michango mbalimbali aliyonipa hadi kufikia kufanikisha kazi hii. Miongozo yake ni muhimu sana na imeifikisha kazi hii katika sehemu iliyotarajiwa.

Tatu, napenda kuwashukuru walimu wangu wote walionisomesha katika viwango mbalimbali kutoka shule ya msingi hadi nilipofikia. Vilevile, natoa shukurani maalumu kwa wahadhiri wa ngazi ya uzamili kwa juhudini zao za kutoa taaluma iliyionongoza kufikia hatua hii.

Shukurani za kipekee ziende kwa mume wangu mpenzi, Bw. Ameir Suleiman Bakar, kwa kunivumilia kwa wakati wote ambao sikuwepo nyumbani, kuishughulikia familia yetu katika kipindi hicho kigumu na kunipa moyo wa mafanikio katika masomo. Nawashukuru pia watoto wangu, Suleiman na Musharaf, kwa kunivumilia katika kipindi chote cha masomo.

Shukurani za dhati pia ziwaendee wote walionisaidia kwa karibu sana katika utendaji wa kazi hii wakiwemo, Mwl. Gora A. Haji, Ussi J. Ussi, wazee na vijana wa Makunduchi, walimu na wanafunzi wa Skuli za Makunduchi na wataalamu wa lahaja. Nilipenda niwataje wote bali nafasi haikutosheleza. Wote hao wamesaidia kunipatia data, muongozo, kunisaidia kimawazo na kunipa moyo wa kuifanya kazi kwa ufanisi. Nathamini sana mchango wao.

Mwisho nawashukuru wanafunzi wenzangu wote ambao tulikuwa pamoja na kusaidiana katika masomo na ushauri wa mambo mbalimbali. Napenda nimtaje bi Sabrina Issa kwa niaba ya wote waliobaki. Ushirikiano wa watu wote hao ndio uliosaidia mafanikio ya kila mmoja wao. Naomba Mwenyezi Mungu awalipe wote hao kila la kheri na mafanikio mema.

## **IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza Athari ya Kiswahili Sanifu katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti ulikuwa na lengo la kutathmini athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi. Ili kukamilisha lengo hilo, utafiti uliongozwa na malengo mahsus matatu, ambayo ni; Kubainisha njia zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu, kubainisha msamiati ulioachwa na ulioibuka kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi. Na, kutathmini athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Mwathiriano wa lugha. Nadharia hii ilitosheleza katika ukusanyaji wa data na uchambuzi wake. Pamoja na nadharia hii, utafiti ultumia mbinu zilizowezesha kukusanya data na kuzichambua. Mbinu hizo ni, hojaji, mahojiano, mjadala wa vikundi na ushuhudiaji. Mbinu na nadharia hii, zilimuezesha mtafiti kujua namna ya upatikanaji wa data, kuzikusanya na kuzichambua hadi kukamilika kwa kazi nzima. Matokeo ya utafiti yalipatikana kutokana na data zilizokusanya kutoka maktabani na uwandani. Matokeo hasa ya uwandani yalitoa jibu la tatizo lililokuwa likishughulikiwa kwa usahihi zaidi. Hii ni kwa sababu mtafiti alifika katika sehemu husika ambako Kimakunduchi kinazungumzwa. Matokeo ya utafiti yaligundua kuwa, kuna baadhi ya msamiati wa kale ambao kwa sasa umeachwa au hutumika kwa nadra kutokana na muingiliano wa Kiswahili sanifu katika lahaja hii. Vilevile, kuna msamiati ambao umeibuka katika lahaja ya Kimakunduchi, msamiati huu haukuwa ukitumika katika lahaja ya Kimakunduchi hapo kabla. Sababu kuu ya kuibuka ni muingiliano wa Kiswahili sanifu kutokana na njia mbali mbali ikiwemo shughuli za kiuchumi, utamaduni na masuali ya kijamii. Kutokana na matokeo hayo, mtafiti aligundua kuwa kuna athari nyingi za muingiliano huu ikiwemo; kupotea kwa msamiati wa asili wa lahaja ya Kimakunduchi na kupoteza vyanzo vyaya msamiati kwa lugha ya Kiswahili sanifu. Hali hii itaifanya lahaja ya Kimakunduchi kuwa hatarini kupotea au kufa kabisa. Mwisho, utafiti umetoa mapendekezo ambayo yataisaidia lahaja ya Kimakunduchi kubaki hai, kujiimarisha na kukiimarisha Kiswahili kwa kikitunzia vyanzo vyake vyaya kuingiza msamiati, kutunza utamaduni na kuchangia utanuzi wa mawanda ya lugha na matumizi yake.

## YALIYOMO

<b>ITHIBATI .....</b>	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TAMKO .....</b>	<b>iv</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>v</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>vi</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>viii</b>
<b>ORODHA YA MAJEDWALI.....</b>	<b>xiii</b>
<b>KIELELEZO .....</b>	<b>xiv</b>
<b>ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA .....</b>	<b>xv</b>
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>1.0    UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
1.1    Usuli wa Mada .....	1
1.2    Tamko la Tatizo la Utafiti .....	4
1.3    Malengo ya Utafiti .....	5
1.3.1    Lengo Kuu la Utafiti .....	6
1.3.2    1Malengo Mahususi .....	6
1.4    Maswala ya Utafiti .....	6
1.5    Umuhimu wa Utafiti .....	6
1.6    Mawanda ya Kitaaluma na Mipaka Yake .....	7
1.7    Muhutasari wa Sura.....	8
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>9</b>
<b>2.0    MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .....</b>	<b>9</b>
2.1    Utangulizi .....	9

2.2	Kazi Tangulizi Kuhusu Dhana ya Lahaja Kwa Jumla .....	9
2.3	Kazi Tangulizi Kuhusu Lahaja ya Kimakunduchi .....	13
2.4	Kazi Tangulizi Kuhusu Kuathiriana kwa Kiswahili Sanifu na Lahaja Zake .....	16
2.5	Mkabala wa Kinadharia /Kiunzi cha Nadharia .....	24
2.5.1	Misingi ya Nadharia za Utafiti .....	26
2.6	Pengo la Utafiti .....	26
2.6.1	Muhtasari wa Sura.....	27
	<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>29</b>
<b>3.0</b>	<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>29</b>
3.1	Utangulizi.....	29
3.2	Mpango wa Utafiti .....	29
3.3	Eneo la Utafiti .....	30
3.4	Jamii ya Watafitiwa.....	31
3.4.1	Kundi Lengwa .....	31
3.5	Sampuli na Usampulishaji .....	32
3.5.1	Sampuli ya Utafiti .....	32
3.5.2	Usampulishaji.....	33
3.6	Mbinu za Utafiti .....	35
3.6.1	Mahojiano.....	35
3.4.1	Mjadala wa vikundi .....	36
3.4.2	Ushuhudiaji .....	37
3.4.3	Hojaji.....	37
3.5	Usanifu wa Utafiti .....	38

3.6	Mbinu za Kuchambua Data.....	39
3.7	Muhtasari ya Sura .....	39
<b>SURA YA NNE.....</b>		<b>40</b>
<b>4.0</b>	<b>UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI.....</b>	<b>40</b>
4.1	Utangulizi.....	40
4.2	Njia Zinazotumika Kuathiri Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi Kutokana na Maingiliano ya Kiswahili Sanifu.....	41
4.2.1	Mwingiliano Kuptia Vyombo vya Habari.....	41
4.2.2	Mwingiliano Kupitia Elimu .....	43
4.2.3	Mwingiliano Kupitia Utamaduni .....	44
4.2.4	Mwingiliano Kupitia Biashara .....	45
4.2.5	Mwingiliano Katika Uhamiaji na Uhamaji .....	47
4.2.6	Mitando ya Kijamii na Vyombo vya Mawasiliano .....	48
4.3	Msamiati Usiotumika na Ulolioibuka Kutokana na Maingiliano ya Kiswahili Sanifu Katika Lahaja ya Kimakunduchi .....	49
4.3.1	Msamiati Ulolioachwa na Ulolioibuka Katika Uwanja wa Elimu .....	50
4.3.2	Msamiati Ulolioibuka na Ulolioachwa Katika Uwanja wa Utamaduni .....	53
4.3.3	Msamiati Ulolioibuka na Ulolioachwa Katika Makundi ya Kijamii.....	56
4.3.4	Msamiati Ulolioibuka na Ulolioachwa Katika Uga wa Habari .....	60
4.4	Athari za Kiswahili Sanifu Katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi .....	61
4.4.1	Kupotea kwa Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi.....	62
4.4.2	Kupoteza Vyanzo vya Msamiati wa Kiswahili Sanifu.....	65
4.5	Muhtasari wa Sura.....	66

<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>68</b>
<b>5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>68</b>
5.1 Muhtasari .....	68
5.1.1 Muhtasari wa Jumla .....	68
5.1.2 Muhtasari Wa Matokeo ya Utafiti.....	69
5.2 Hitimisho.....	71
5.3 Mapendekezo .....	72
5.3.1 Mapendekezo ya Kukabiliana na Changamoto Zilizobainika Katika Utafiti Huu.....	72
5.3.2 Mapendekezo Kwa Tafiti Zijazo.....	74
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>75</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>78</b>

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 3.1: Mgawanyiko wa Sampuli ya Watafitiwa .....	33
Jedwali 4.1: Msamiati Ulloibuka Katika Uwanja wa Elimu	52
Jedwali 4.2: Maneno ya Kiswahili Sanifu Yanayotumika Katika Nyimbo za Michezo ya Watoto za Lahaja ya Kimakunduchi.....	55
Jedwali 4.3: Msamiati Ulloachwa Katika Sherehe za Harusi .....	56
Jedwali 4.4: Msamiati Ulloachwa Katika Miiongoni mwa akina Mama.....	57
Jedwali 4.5: Msamiati Ulloachwa Miiongoni mwa vijana .....	59

## **KIELELEZO**

Kielelezo 3.1: Ramani ya Kisiwa cha Unguja Inayoonesha Eneo la Utafiti..... 31

**ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

BAKIZA	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
Bi	Bibi
Bw.	Bwana
Dkt.	Daktari
Ht	Haina tarehe
Mw.	Mwalimu
Na.	Namba
NKM	Nadharia ya Kidhi ya Mawasiliano
S.W	Subhaana Wataala
SUZA	<i>The State University of Zanzibar</i>

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### **1.1 Usuli wa Mada**

Lugha ni mfumo wa mawasiliano ambao hukua na kubadilika kulingana na maendeleo ya watumiaji wa lugha hiyo. Nassor, (2001) anadai kuwa lugha huweza kukua hatua kwa hatua na kufikia kilele cha kimaendeleo na kuwa lugha ya Kimataifa, kama ilivyo lugha ya Kiingereza. Pia, lugha huweza kudumaa hadi kufikia kufa kabisa kwa lugha hiyo. Ukuaji wa lugha au kufa kwa lugha kunatokea kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mfano lugha hukua kutokana na kuongezaka kwa msamati na idadi ya wazungumzaji. Kufa kwa lugha vilevile hutokea kutokana na kukosa kuongeza msamati unaoendana na wakati na kupungua kwa wazungumzaji wanaoutumia kama lugha mama hatua kwa hatua hadi kumalizika kabisa wazungumzaji wa lugha hiyo.

Kiswahili ni lugha ambayo ina asili ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki, kwa mujibu wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988), wanadai kuwa Waarabu walipofika sehemu mbalimbali za ukanda wa pwani mnamo karne ya 10 BK walizikuta lugha hizi na walizijumuisha na kuziita “Sawahil” yaani lugha za pwani, kutokana na athari za kimatamshi neno hilo baadaye lilbadilika na kuwa Ki-swahili. Lugha ya Kiswahili imejumuisha lahaja nyingi ndani yake, kama vile Kiunguja, Kingome, Kikomoro, Kipemba, Kitumbatu, Kimakunduchi, Kimvita, Kisiu, Kisabaki, na Kiamu.

John na Mduda (2011) wanasema kuwa lahaja ni vilugha ambavyo vina chimbuko

moja, hivyo vinafanana kwa kiasi kikubwa katika vipengele mbalimbali nya lugha. Kipacha, (2003) anaeleza kuwa dhana ya lahaja ni namna ya uzungumzaji unaotambulisha kundi jamii fulani mabsusi na pia ni namna ambazo huweza kutofautisha kati ya kundi jamii moja na jingine. Tofauti hizo huwezesha kupambanua kwa mfano kati ya Mpemba na Mtumbatu au Mvita na Mbarawa. Kwa walio wengi dhana ya lahaja huchukuliwa kama kinyume cha lugha sanifu.

Lahaja ni tofauti zilizomo ndani ya lugha kuu moja ambapo watumiaji wa eneo moja hutofautiana na watumiaji wa eneo jengine kimatamshi, kimuundo na kimaana. Pia zipo lahaja ambazo zinatokana kwa matabaka mbali mbali ya watu katika jamii. Lahaja ambazo huzuka kutokana na kuzungumza na watu wanaoishi katika eneo moja la kijografia lakini huwa wametengana kwa milima au kisiwa (Mhilu na wenzake, 2010). Kuna lahaja zisizopunguwa kumi na tano katika Kiswahili ambazo ni Kipemba, Kitumbatu, Kimakunduchi, Kimrima, Kingao, Kimtang'ata, Kivumba, Kipate, Kimvita, Kisiu, Kituku na Chambalazi.

Katika mjumuiko huo wa lahaja za Kiswahili, kulikuwa na matumizi ya aina tofauti za lahaja katika msamiati, matamshi au muundo wa sentensi zake. Kwa hivyo kulikuwa na haja ya kuwa na lugha sanifu ambayo itaweza kuwa ni lugha ya mawasiliano na kutumiwa katika shule. Mganga (1997) anaeleza kuwa kamati ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili, baada ya kujadili kwa kina na katika mikutano yake mbali mbali, ilikichagua Kiunguja kuwa ni lahaja ya kusanifishwa na kutumika rasmi katika mawasiliano rasmi na ufundishaji katika shule. Usanifishaji haukuwa na maana kuwa huo ulikuwa ndio mwisho wa lahaja nyingine za Kiswahili, hasa, lahaja

ziliendelea na kuwa ni chanzo muhimu cha kukuza msamiati wa Kiswahili sanifu. Miongoni mwa lahaja hizo kilikuwa ni Kimakunduchi.

Msingi mkuu wa msamiati katika lugha sanifu ni kutoka katika lahaja mbalimbali zinazotoka katika kundi lahaja za Kiswahili. Lahaja tofauti zimechangia msamiati, lafudhi na mitindo. Lahaja hizi huweza kutofautiana katika kiwango cha uchangiaji wa msamiati huo. Massamba (2006:56) anaeleza kuwa, “Msamiati ni jumla ya maneno yatumikayo katika lugha”. Hii ina maana kuwa msingi mkuu au uhai wa lahaja au lugha yoyote ni msamiati. Kwa mantiki hiyo lugha hukua kwa kuongeza msamiati kwa njia mbalimbali, ikiwemo ya kuchukua katika lahaja zake. Na hii ndio njia kuu ya kuongeza msamiati katika lugha sanifu, ili kukidhi mahitaji ya kimawasiliano. Lugha inapochukua msamiati kwa wingi katika lahaja fulani huweza kuiathiri zaidi lahaja hiyo kuliko nyingine, hadi kufikia kufa kabisa kwa lahaja hiyo kutokana na mfanano mkubwa wa lahaja husika na lahaja sanifu.

Kimakunduchi ni lahaja inayojulikana kwa majina mbalimbali kama vile, Kikale, Kihadimu au Kikae. Kimakunduchi huzungumzwa sehemu za kusini na mashariki ya Kisiwa cha Unguja umbali upatao maili 40 kutoka mji wa Zanzibar. Makunduchi, kietimolojia ni sehemu ya udongo mwekundu, jamii hii inamkusanyiko wa vijiji ingawaje wenyeji hupenda kujita wahadimu. Maeneo makuu yanayozungumza lahaja ya Kimakunduchi ni pamoja na sehemu za Bwejuu na Jambiani kwa upande wa pwani na Kaskazini ya Makunduchi. Upande wa Magharibi, huzungumzwa katika sehemu za Kizimkazi na Muyuni na katika kisiwa cha Uzi. Pamoja na sehemu

nyingine zilizopakana na maeneo haya. Kwa jumla lahaja hii inajulikana kuwa inazungumzwa katika Mkoa wa Kusini Unguja.

Kimakunduchi ni lahaja inayozungumzwa kusini mwa kisiwa cha Unguja,. Lahaja hiyo ina mitindo na aina zake za uzungumzaji. Lahaja hiyo ina msamati mwingi ambao haupatikani katika Kiswahili sanifu na ina namna yake ya utamkaji. Kutokana na hali hiyo, kuna watu huamini kuwa Kimakunduchi si Kiswahili kama ilivyobainishwa na Mohammed (2013) alipomnukuu Rais wa nne wa Zanzibar aliposema kuwa kwa sababu hiyo baadhi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili.' Imani hiyo imetokana na namna ya msamiti na namna ya uzungumzaji wa watu wa lahaja hiyo.

## **1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Lugha ya Kiswahili imekuwa na uenezi mkubwa duniani. Kupanuka kwa lugha hii kumetokana na kutumika kwake katika nyanja mbalimbali za kimaisha pamoja na maendeleo ya kiulimwengu. Mjawiri (2016) anaeleza kuwa vyombo vyahabari kama ni sehemu ya utandawazi kwani ndivyo vilivyokuza msamati, istilahi na mitindo ya lugha ya Kiswahili na kuifanya lugha hii ivume, inawiri, na itambulike duniani kote. Kutokana na lugha sanifu ya Kiswahili kutumika katika shughuli zote rasmi kama ilivyobanishwa na Mganga (keshatajwa) kuwa Kiswahili Sanifu kilichofanywa na watu hao (waliosanifisha lugha) ndicho kilichokubalika na serikali na kutumika katika shughuli rasmi kama vile elimu, utawala, mahakama na katika mikutano ya hadhara.

Hata hivyo, pamoja na matumizi hayo makubwa ya Kiswahili sanifu, lahaja za lugha hiyo zilibaki na matumizi yake katika jamii za watu wanaohusika nazo. Muathiriko wa muingiliano kati ya Kiswahili sanifu na lahaja zake kama vile Kimakunduchi, unachukuwa nafasi kubwa ya kuathiri lahaja hizo kiisimu. Kama asemavyo Mbiti (1969: 216), “hakuna watu au nchi ambayo inaweza kubaki nyuma au kutoathiriwa na mabadiliko mapya ya Sayansi na Teknolojia”. Kwa msingi wa kauli hiyo, ni dhahiri kwamba maendeleo yanayojitokeza kwa kasi kila siku katika Kiswahili sanifu yanaweza kuziathiri lahaja za lugha hiyo. Miongoni mwa kazi zilizojikita moja kwa moja katika kuangalia athari za muingiliano katika lugha ni pamoja na Stigand, (1915), kati kuliangalia suali hili alijaribu kuandaa msamiati wa lahaja mbali mbali za Kiswahili pamoja na matamshi yake. Lahaja za Zanzibar kama vile lahaja ya Kimakunduchi imekuwa karibu sana kimaingiliano na Kiswahili Sanifu, ambacho kinazungumzwa Mjini Unguja. Hali hii inatokana na shughuli mbali mbali za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimazingira zinazifanya jamii mbili hizi kuingiliana sana na kwa karibu zaidi. Hali hii inatishia uhai na maendeleo ya lahaja ya Kimakunduchi.

Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kubaini athari za Kiswahili sanifu zilizojitokeza kwa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo katika nyanja zote za kimaisha.

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu na malengo mahsus iyalivomuongoza Mtafiti katika kazi hii

### **1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti**

Kutathmini Athari za Kiswahili Sanifu katika msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi.

### **1.3.2 1Malengo Mahususi**

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi yafuatayo:

- i) Kuchambua njia zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu.
- ii) Kubainisha msamiati ulioachwa na ulioibuka kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi
- iii) Kutathmini athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi

### **1.4 Maswala ya Utafiti**

Katika kufikia malengo ya utafiti, Mtafiti aliongozwa na maswali yafuatayo:

- i) Ni njia gani zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu?
- ii) Ni msamiati upi ulioachwa na ulioibuka kutokona na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi?
- iii) Kuna athari gani za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi?

### **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Baada ya kukamilika kwa utafiti huu, kazi hii itasaidia kutoa mwanga kwa wanataaluma wa isimu kwa kuelewa msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi

ulioongezeka na ule ulioachwa kutokana na mwingiliano wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi.

Pili, utafiti huu utafunua macho kwa wanalahaja kujua mabadilko ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi yaliyotokana na mwingiliano na Kiswahili sanifu. Hali hii itabainika baada ya kulinganisha na etimolojia halisi ya maneno hayo na kuangalia maana ya zamani na maana inayotumika katika wakati hui.

Pia, utafiti huu unategemewa kuwa nguzo ya wanaisimu kujua mwelekeo wa lahaja ya Kimakunduchi na lahaja za Kiswahili kwa jumla kutokana na mabadiliko yanayotokea katika lahaja hizo kutokana na mwingiliano wa Kiswahili sanifu kwa lahaja hizo. Suala hili litakuwa muhimu kwa watunga sera hasa ya lugha ya Kiswahili, kwa kupata mwelekeo halisi wa lugha ya Kiswahili kupitia lahaja zake na kupanga namna ya kukabiliana na mabadiliko hayo.

### **1.6 Mawanda ya Kitaaluma na Mipaka Yake**

Mtafiti alikusudia kuchunguza juu ya athari ya Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi. Mtafiti alichunguza zaidi katika kipengele cha msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kwa kuangalia mambo matatu makuu;

Kwanza, utafiti ulijikita katika kuangalia mabadiliko ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kwa kulinganisha na maana ya asili na ile maana iliyoibuka kutokana na maendeleo yaliyojitokeza katika Kiswahili sanifu.

Pili, utafiti ulijikita katika kuangalia msamiati ulioachwa kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi, msamiati huo ama hautumiki au haupo katika hali yake ya uhalisia.

Mwisho utafiti ultathmini athari za Kiswahili sanifu katika kuuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maendeleo yanayoshamiri kila siku katika Kiswahili sanifu. Kwa jumla utafiti ulijikita na msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi na athari zake zinazotokana na mwiningiliano na Kiswahili sanifu. Lahaja ya Kimakunduchi iliyofanyiwa kazi katika utafiti huu ni ile lahaja ambayo inazungumzwa eneo la Mkoa wa kusini Unguja na hasa katika kijiji cha Makunduchi.

### **1.7 Muhutasari wa Sura**

Sura hii ni sura ya utangulizi ambayo imebainisha usuli wa mada na kutoa dhana ya utafiti kwa jumla, vilevile imeonesha tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na masuali yaliyoongoza utafiti huu. Sura hii pia imeonesha umuhimu wa utafiti, mawanda ya kitaaluma ya utafiti na mipaka yake. Sura inayofuata ni mapitio ya maandiko tangulizi yanayohusiana na mada au mbinu zilizotumika.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii ni mapitio ya machapisho ya kazi tangulizi zilizo zungumzia juu ya mada, zinazolingana au kukaribiana na mada iliyofanyiwa utafiti pamoja na kuangalia nadharia iliyotumika. Mapitio mbali mbali yamechambuliwa ili kutoa ufanuzi wa kina juu ya athari ya namna Kiswahili sanifu kilivyoithiri lahaja ya Kimakunduchi. Vipengele mbali mbali vya lugha pamoja na tafiti zilizofanywa kuhusiana na lahaja ya Kimakunduchi zilipitiwa ili kupata muangaza wa jumla kwa namna gani watafiti walivyoiangalia lahaja ya Kimakunduchi pamoja na athari za Kiswahili sanifu kwa lahaja hiyo. Pia, mtafiti ameeleza nadharia na misingi yake iliyotumika katika kukusanya na kuchambulia data za utafiti huu.

#### **2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Dhana ya Lahaja Kwa Jumla**

Dhana ya lahaja ni dhana pana sana yenye mitazamo tofauti kulingana na wataalamu. Kwa upande wa Kipacha, (2003) anaeleza kuwa, lugha huweza kuwa na namna tofauti tofauti za usemajji, lafudhi na hata utumiaji tofauti wa maneno katika sehemu mbalimbali za wazungumzaji wanaojihesabu kuwa wanazungumza kundi-lugha fulani. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa katika lugha moja kuna tofauti kadha za matamshi, msamiati na mtindo wa usemajji mambo ambayo hutofautiana katika hali ya makundi na kuitwa kundi-lugha. Bila ya shaka kwa dhana hii tunaweza kusema kuwa kundi-lugha ina maana ya lahaja katika lugha fulani. Massamba na wezake, (2001) wakichambua dhana ya lahaja wanaeleza kuwa; lahaja ni mojawapo kati ya

lugha ambazo kusema kweli huhesabika kama lugha moja ispokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele fulani fulani, kama vile lafidhi, fonolojia, msamiati usiokuwa wa msingi au miundo. Maana hii inatiliwa nguvu na Kipacha, (keshatajwa) anasema kuwa fasili ya dhana ya lahaja ipo katika mtazamo miwili; mtazamo pungufu na mtazamo wa uelewano. Kwa kuanzia na mtazamo pungufu, inaelezwa kuwa; lahaja ni ki-lugha ambacho hakiandikwa kisicho na maandishi. Mtazamo huu, unapambanua lahaja na lugha kwa kuangalia kipengele cha ukubwa na umaarufu. Lugha huonekana ni kubwa na lahaja ni ndogo. Katika mtazamo huu pia lugha huchukuliwa kuwa ni yenyе hadhi zaidi kuliko lahaja. Lugha ni ile inayotumika katika shughuli rasmi kama vile kama vile kutolea elimu, kutumika maofisini, mahakamani pamoja na sehemu nyingine rasmi. Dhana hii pia inatilia nguvu katika lugha kwa kunasibishwa na maandishi wakati lahaja inawekwa katika fungu la mawasiliano yasiyo na maandishi. Kwa jumla vigezo hivi si vya msingi kwa sababu lahaja za Kiswahili ni lahaja zilizokatika maandishi kwa njia mbalimbali. Ni wazi kuwa hatuwezi kutumia dhana hiyo kwa sababu lugha ni zao la lahaja, na sikila lugha isiyo na maandishi katika eneo husika huweza kuwa lahaja ya lugha inayozungumzwa katika taifa hilo. Mfano Tanzania lugha inayotumika ni lugha ya Kiswahili ila si kila kundi-lugha linalozungumzwa hapa ni lahaja ya Kiswahili. Mfano, Kimasai, Kinyamezi na lugha nyingine za kikibili si lahaja za lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa mtazamo wa Uelewano, Kipacha (keshatajwa) anaeleza kuwa; lahaja ni lugha yoyote ile iwe imeandikwa au haijaandikwa. Kwa maana kuwa lahaja ni sehemu ya kundi-lahaja ambalo linajulikana kama ni lugha fulani. Kwa mfano

tunaposema lugha Kiswahili tunakusudia kuwa ni kundi-lahaja za Kiswahili. Na inaposemwa lugha sanifu ni ile lahaja inayotoka katika kundi-lahaja fulani na kusanifiwa ili kuwakilisha kundi-lahaja izo katika shughuli rasmi za Kitaifa. Hivyo Kiswahili sanifu ni lahaja ya Ki-unguja mjini kilichosanifiwa kwa ajili ya kuwakilisha kundi-lahaja za Kiswahili ili kutumika katika shughuli rasmi za kitaifa kama vile elimu, ofisini, mahakamani na sehemu nyingine kama hizo. Dhana hii inajumuishwa kwa fasili inayosema kuwa; lahaja ni matokeo ya lugha kuwa na launi kadhaa zinazowabainisha watumiaji wake mahali watokapo au tabaka lao. Tofauti za launi hizo haziathiri maelewano baina ya mifumo na kanuni-miundo ya lahaja hizo. Kipacha (keshatajwa) anachambua zaidi kwa kusema; lahaja hugawanyika katika makundi mawili makuu. Lahaja ya Kijiografia na lahaja ya kijamii. Wazungumzaji wawili wa lugha moja wanaweza kutofautiana baina yao kwa vile wanatoka sehemu mbalimbali au wakatofautiana kwa vile wanatoka katika matabaka tofauti. Namna ya kuzungumza kwa watu hao kutatofautiana kwa kiasi fulani kidogo (hasa matamshi au msamiati). Maelezo haya yanaweza kusaidia kazi hii kujumuisha dhana ya lahaja kwa kusema kuwa; Lahaja ni kitarafa cha lugha kinachobainika kijamii au kijiografia na kudhihirishwa na vipengele maalumu vya kisauti na kimuundo.

Moja mionganoni mwa sifa ya lugha ama lahaja ni kuwa na uwezo wa kupokea msamiati kutoka katika lugha au lahaja mbalimbali. Kutokana na imani hiyo, Lahaja ya Kimakunduchi nayo imechukuwa msamiati kutoka katika Kiswahili sanifu na kuiathiri lahaja hiyo. Kipacha, (2004) akichambua zaidi kuhusu lahaja anasema kuwa kazi ya kwanza kabisa ya utafiti wa lahaja za Kiswahili iliandikwa mwanzoni mwa karne ya<sup>19</sup> ili kuweza kufahamu lugha za wenyoji wa pwani na kurahisisha shughuli

za kiuchumi, dini, na utawala. Lahaja kadhaa zimechunguzwa kama Kimtangata (Whiteley, 1988), Chichivundi (Lambati, 1958) na Kipemba (Whiteley, 1985). Mwishoni mwa karne ya 20 walijitokeza wazawa wa lugha na kuendeleza kazi ya uchunguzi kwa kuchunguza lahaja za Kiswahili kwa kuendeleza kazi zilizofanywa na watafiti wengine kama vile Mshindo (1989), Batibo (1982), na Khamisi (1984) waliofanya tafiti za Kiswahili. Baadhi yao wamechunguza vipengele vya sarufi za lahaja hizo huku wakilinganisha na vile vya Kiswahili kazi za watalamu hawa zimetoa mwangaza kwa mtafiti kwa kumsaidia kufahamu lahaja mbalimbali za Kiswahili ikiwemo lahaja ya Kimakunduchi.

Muhidin (2010) akichambua kuhusu lahaja zinazopatikana Zanzibar, anaeleza kuwa Kiswahili ni lugha pekee inayozungumzwa na Wazanzibari, ila hutofautiana katika uzungumzaji kwa mujibu wa mgawanyiko wa maeneo ambamo tunapata lahaja mbalimbali kama vile Kihadimu (lahaja za kusini Unguja kikiwemo Kimakunduchi), Kipemba, Kitumbatu na Kiunguja Mjini. Kiunguja Mjini ni lahaja iliyoteuliwa na Wazungu Wakoloni kuwa kigezo cha kukisanifisha Kiswahili tokea mwaka 1930 (Masebo & Nyangwine, 2007). Lahaja Sanifu ni lahaja ambayo imefanyiwa marekebisho ya matamshi, sarufi na maana kutoka katika lahaja za lugha ili kutumika katika shughuli zote rasmi (Massamba, 1990:53).

Naye Whiteley (1954) alifanya utafiti kuhusu laahaja ya Kimtangata, akieleza zaidi matamshi ya lahaja ya Kimtangata na kugusia zaidi juu ya sifa za lahaja zenye kutofautiana baina ya lahaja moja na nyingine pia amechunguza mambo yaliyo mahsusni katika kila lahaja. Kwa mfano amechunguza juu ya mashina ya maneno.

Kazi hii ilimsaidia mtafiti kwa kupata muongozo wa kufahamu sifa za lahaja ambazo zilimuongoza mtafiti kuzifahamu sifa zinazoonesha namna lahaja zinavyoweza kuathiriana na lahaja ambayo itakuwa na matumizi na mawanda mapana zaidi kuliko lahaja nyingine. Kama ambavyo utafiti huu umelenga, mtafiti alipata kuona ni kwa namna gani lahaja zenyе nguvu za matumizi na mawanda ya kimsamiati na eneo la watumiaji ina nafasi kubwa kuchukuwa nafasi ya mawasiliano kuliko lahaja ambazo zina ufinyu wa matumizi.

Shgand (1915:2-3) anaeleza lahaja tofauti za Kiswahili naye anataja lahaja 15 ambazo ni Kiunguja, Kimrima, Kimgao, Kibadani, Kipemba, Kimvita, Kivumba, Kimakunduchi, Kipate, kisiu, Kingazija, Kitikuu, lahaja zote hizo zimetawanyika maeneo tofauti ya Upwa wa Afrika ya mashariki. Kazi hii ilimsaidia sana mtafiti katika kufanya uchunguzi wake juu ya lahaja ya Kimakunduchi kwani mtafiti atapata kufahamu misamiati tofauti ya lahaja ya Kimakunduchi na kuweza kugundua jinsi gani misamiati hiyo inavyoathirtiwa na muingiliano wa Kiswahili sanifu.

Kwa jumla maandiko haya yametoa mwangaza wa kufahamu dhana ya lahaja kwa mujibu wa mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Hali hii itamsaidia mtafiti kutofautisha kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu (Kilahaja Sanifu). Lengo ni kuchambua athari za Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi.

### **2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Lahaja ya Kimakunduchi**

Wataalumu wengi waliochambua lahaja za Kiswahili wamethibitisha kuwa lahaja ya Kimakunduchi ni mionganoni mwa lahaja za kundi lahaja za Kiswahili. Kutohana na

hili hiyo, wapo watafiti mbalimbali waliojikita katika kutafiti na kuchambua lahaja ya Kimakunduchi. Kwa upande wa Juma, (2011) alifanya ulinganishi wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu, na Kizimkazina akagundua kuwa kuna uhusiano wa kihistoria wa kimsamiati unaotumika na wenyeji wa Makunduchi, Bwejuu, Kizimkazi, na Jambiani. Kwa kuititia kazi hii mtafiti alipata msaada wakati wa kukusanya data kwa kuweza kuijua asili ya misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi na eneo ambalo mtafiti pia aliweza kulitembelea na kupata kukusanya data zilizosaidia kujua upana wa eneo la lahaja ya Kimakunduchi.

Maganga (1991) alishughulikia lahaja tatu kuu za Zanzibar ambazo zinazpatikana katika visiwa vyote viwili vikubwa vya Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Lahaja zilizoshughulikiwa ni Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu kwa kuzihusianisha na Kiswahili sanifu. Katika tasnifu hiyo, mtafiti alilenga kuchunguza mofofonolojia ya lahaja za Kipemba, Kitumbatu, na Kimakunduchi huku akizihusianisha na Kiswahili Sanifu. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kupata baadhi ya misamiati ultumika katika lahaja tofauti na kutiliwa mkazo zaidi msamiati wa Kimakunduchi. Kazi hiyo pia ilitoa mwongozo wa ukusanyaji na uchambuzi wa data zake.

Maganga (1997) alizitaja lahaja mbali mbali za kusini na kaskazini, na kueleza jinsi lahaja zinavyotofautiana kati yao. Katika kielelezo cha lahaja mama ya kusini, amekionyesha Kimakunduchi na hivyo, kumwezesha mtafiti kuelewa asili ya lahaja aliyoifanyia utafiti. Maganga (keshatajwa) amefanya uchunguzi wa fonolojia na kimofolojia katika lahaja ya Kiunguja mjini, Kimakunduchi, Kipemba na Kitumbatu. Utafiti wake juu ya lahaja ya Kimakunduchi amegundua kuwa maneno

katika nyakati tofauti yanatumia viambishi tofauti na Kiunguja mjini akatoa baadhi ya maneno hayo ni kama:

<b>Kimakunduchi</b>	<b>Kiunguja mjini</b>
Nyona	nilionna
Nyuza	niliuza
Nyiuzu	niliuliza
Nisumku	nilikumbuka

Utafiti wa Maganga umetoa hamu ya kutaka kufahamu zaidi juu ya misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi na kutohana na kuwa Maganga hakuchunguza ni kwa jinsi gani misamiati hiyo inavyoweza kuathiriwa na mwingilio wa Kiswahili sanifu. Mtafiti ameona ipo haja ya kufanya uchunguzi huo kwa kina zaidi.

Kipacha (2002) alichunguza lahaja za Kiswahili zilizomo ndani ya Afrika ya Mashariki kama vile Chimwinyi, Kitukuu, Kipate, Chijomvi, Kingare, Kisiu, Kiamu, Kivumba, Kimrima, Kipemba, Kiunguja, Kimakunduchi, Kimgao, na Kitumbatu. Katika uchunguzi wake alijikita zaidi katika kipengele cha msamiati na kwa kiasi kidogo aligusia vipengele vya kifonolojia na miundo pia kazi hiyo inaonyesha vipengele mbali mbali vya kiisimu katika lahaja ya Kimakunduchi na zaidi kulinganisha msamiati wa lahaja kuu za Kiswahili. Kazi hii ya Kipacha ilimsaidia sana mtafiti kufahamu misamiati ya lahaja za Kimakunduchi asilia na kuweza kugundua athari zilizopatikana kutohana na athari za Kiswahili sanifu. Kazi ya Kipacha pia ilisaidia kuona msamiati ambao hautumiki kwa mujibu wa uasili wa Kimakunduchi au umekuwa na matumizi tofauti au kusahaulika kabisa. Yote hayo ni matokeo ya athari iliyosababishwa na mwingiliano wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu kilichotawala katika nyanja zote za maisha.

## **2.4 Kazi Tangulizi Kuhusu Kuathiriana kwa Kiswahili Sanifu na Lahaja Zake**

Wataalamu mbalimbali wamekubaliana kuwa lahaja na lugha kwa jumla huathiriana baina yao. Lahaja mionganoni mwa kundi lahaja moja huweza kuathiriana baina yao, lahaja za makundi lahaja tofauti huweza kuathiriana baina yao na lugha mbili tofauti huweza kathiriana baina yao kama zilivyo lugha ya Kiarabu na lugha ya Kiswahili katika suala la msamiati. Ipo mitazamo finyu ya kudhofisha lahaja kama anavyooleza Mbabu (2003), kwa kusema kuwa, lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kiasi kwamba zile zinazofahamika kwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili ni chache tu kutokana na kutozitafiti vya kutosha. Anaendelea kueleza kwamba, jambo lililowafanya wataalamu hao wa Kiswahili kutozitafiti lugha hii kwa upana unaostahiki ni dhana kwamba Kiswahili Sanifu ndiyo hasa Kiswahili chenyewe na hivyo kupuuzia lahaja mbalimbali za Kiswahili. Jambo hilo huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuziathiri lahaja kimsamiati. Athari za Kiswahili sanifu kwa lahaja zinakuwa na nguvu zaidi kutokana na mawanda ya matumizi na watumizi wa Kiswahili sanifu. Maelezo haya yametupatia changamoto na chachu ya kufanya utafiti wa kina ili kuona lahaja ya Kimakunduchi imeathirika kwa kiasi gani kutokana na mwingiliano uliopo kutokana na Kiswahili sanifu.

Majawiri (2016), akieleza njia zinazotumika kuathiri lahaja katika jamii ya Zanzibar, anaeleza kuwa vyombo vya habari kwa upande wa Zanzibar vinaendeleza msamiati, istilahi na mitindo ya lugha ya Kiswahili. Vyombo hivi vilisaidia na vinasaidia lugha ya Kiswahili kuvuma, kunawiri na kutambulika duniani kote. Maelezo haya yanachambua athari za vyombo vya habari katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Ni wazi kuwa jamii za lahaja nyingine zinapojikita katika matumizi ya

lugha sanifu ya Kiswahili ni chanzo cha kupungua nguvu kwa lahaja za jamii hiyo, kutokana na wanajamii kuzoea kutumia msamiati sanifu zaidi na kuacha taratibu kutumia msamiati wa lahaja zao. Pia huwaathiri wanalahaja hao hata katika suala la fonolojia ya lahaja hiyo.

Ali (2016) alifanya utafiti juu ya athari za utandawazi katika lahaja ya Kitumbatu. Katika kazi yake alijaribu kuonesha athari za utandawazi katika lahaja ya Kitumbatu. Amebainisha sababu zinazopelekea mabadiliko ya kiutandawazi katika msamiati wa lahaja ya Kitumbatu. Katika lengo hili alibainisha msamiati uliopotea kutokana na athari za utandawazi katika jamii ya Tumbatu kama vile; Kalyamange, kivumbwe, veveteko, danwa, moko na mengineyo. Kazi hii ilijumuisha kwa kusema kuwa vijana ndio kundi kubwa linaloathiri lugha katika jamii kupitia maendeleo ya kiutandawazi. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa hata uenezi wa utandawazi unakipa nafasi kubwa zaidi Kiswahili sanifu dhidi ya lahaja za lugha hiyo.

Mutembei (2011) alifanya utafiti wa kuchunguza lugha tandawazi, akiwa na shabaha ya kuibua changamoto zinazoletwa na lugha tandawazi katika isimu jamii, hasa kubadili na kuchanganya misimbo na kuhusisha athari zake na vipengele vya isimu jamii. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kuangalia matumizi ya Kiswahili katika simu za kiganjani. Alipendekeza kuwa changamoto zinazoletwa na lugha tandawazi hazina budi kufanyiwa utafiti zaidi ili kubaini mwelekeo wa lugha kama ambavyo lugha inavyotumika katika mawasiliano ya simu za kiganjani. Aliendelea kupendekeza kuwa ufupishaji, udondoshaji tafsiri, kutumia namba na kuchanganya lugha ni mambo ambayo wanaisimu jamii na wanamawasiliano kwa jumla hawana budi

kuyaangalia kwa kina katika lahaja tofauti tofauti, kama ilivyo kwa watumiaji wa Kiswahili na Kiingereza. Mwisho. Mutembe ali sema kuwa utandawazi umeibua mtindo mpya katika Isimu Jamii na waendelezaji wakubwa wa mtindo huo ni vijana, lakini hakushughulikia athari hizo katika Kiswahili cha Tumbatu. Kazi hizi zimetoa mwelekeo wa utafiti huu kwa kuonesha namna utandawazi unavyoathairi lugha na kusababisha baadhi ya msamiati kuachwa na kutokutumika kabisa kama ilivyooneshwa katika utafiti uliofanyika katika lahaja ya Kitumbatu, pia kazi hizi zimetoa majumuisho kwa kueleza vijana ndio jamii kubwa inayopokea mambo ya utandawazi na kusababisha athari katika utamaduni na lugha za jamii zao.

Kutokana na utafiti huo hapo juu, ni dhahiri kuwa kumekuwa na wimbi la uongezekaji wa msamiati katika lahaja unaotokana na matumizi ya zana za kimaendeleo yanayotawaliwa zaidi na lugha sanifu.

Rafi (h.t) aliandikia kuhusu uchambuzi wa matini za ujumbe mfupi katika lugha na jinsia. Lengo kuu la utafiti wake ni kuchunguza uchaguzi wa msamiati na mofosintaksia kwa wanawake na wanaume wanaotumia ujumbe mfupi katika simu ya kiganjani. Vilevile aliangalia athari za Lughatandawazi katika lugha itumikayo katika vyombo vyahabari. Katika utafiti huo zilichukuliwa matini za ujumbe mfupi mia moja katika simu za kiganjani zilizoandikwa na wanaume na wanawake. Matini hizo zilichambuliwa ili kuangalia msamiati, mofolojia na sintaksia ya watumiaji wa ujumbe mfupi na kuangalia athari ya ujumbe mfupi katika biashara.

Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa katika ujumbe mfupi kumekuwa na lugha mpya ambayo inaathiri lugha ya vyombo vyahabari. Vilevile yalionesha kuwa kuna

tofauti za msamiati na mofosintaksia ya wanawake na wanaume katika ujumbe mfupi wa simu za kiganjani. Hata hivyo, utafiti huo haukuhusisha lugha ya Kiswahili na lahaja zake ila imejaribu kugusa msamiati na mabadiliko yake kutokana na athari za mawasiliano. Hivyo maelezo hayo yalikuwa ni muongozo bora wa kazi yatu ambayo ilijikita moja kwa moja katika kuchunguza msamiati ulioachwa na ambo ama unatumika kwa nadra au umeachwa kabisa na nafasi ya msamiati huo kuchukuliwa na msamiati uliotokana na Kiswahili sanifu au kutumika sambamba.

Kwa upande wa Ong'onda na wenzake (2011) waliandika kuhusu vipengele vya kisintaksia katika matini za ujumbe mfupi. Lengo la utafiti wao ni kuchambua vipengele vya kisintaksia vya ujumbe mfupi kwa Wakenya. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa miundo mipyga ya kisintaksia imesambaa kwa kiwango kikubwa katika vipengele vya kiisimu baina ya wakenya wanaotumia njia hii ya ujumbe mfupi. Aidha, uchambuzi ulionesha kuwa umbile la kisintaksia la ujumbe mfupi lipo kwenye sentensi na katika mabadiliko ya neno. Hivyo, linaathiri mabadiliko ya kiisimu na kwa maana hiyo inasababisha lugha kubadilika. Hali kadhalika, matokeo yameonesha kuwa ujumbe huo umegubikwa sana na udondoshaji na vifupisho. Mwisho walieleza kuwa hali hii inasababishwa na mabadiliko ya kijamii.

Utafiti huu, umefanikiwa kuchambua vipengele vya kisintaksia katika ujumbe mfupi, ila hawakueleza ni kwa kiasi gani msamiati wa lugha husika unaathirika kutokana na maendeleo haya ya kimawasiliano. Maelezo haya yanatiliwa nguvu zaidi na Barasa na Mous (h.t) walioandika kuhusu mwiingiliano wa mazungumzo na maandishi katika ujumbe mfupi wa simu za kiganjani wakizingatia mfumo mpya wa teknolojia

ya mawasiliano. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kuchunguza athari za lugha katika kujua kusoma na kuandika katika mfumo mpya wa teknolojia ya mawasiliano. Matokeo yameonesha kuwa kuibuka kwa simu za kiganjani kumeleta muundo mpya wa matumizi ya lugha ambayo yanavuruga lugha sanifu na umesababisha kuwepo kwa tahajia mpya. Mwisho walihitimisha kwa kusema kuwa athari hii ni kubwa kutokana na kuwepo kiwango kikubwa cha watu ambao njia yao maarufu waliyoizoea katika kuwasiliana ni ya utumaji ujumbe. Wamefanikiwa kuonesha athari za ujumbe mfupi katika lugha na hasa katika kipengele cha tahajia ila hawakuweza kuonesha ni kwa vipi hali hiyo inaweza kuathiri msamiati kwa kuachwa au kubadili maana kwa msamiati uliokuwepo.

Wataalamu hao waliotajwa hapo juu, wamebainisha kuwa kumekuwa na kuachwa kwa maneno katika mazungumzo ya watu kulingana na mahitajio ya mawasiliano yao. Utufauti huo hujitokeza kutokana na mwingiliano wa wazungumzaji kutoka katika lahaja tofauti. Wazungumzaji hao hutafuta lugha ama lahaja itakayoweza kuwaunganisha na kuwawezesha kukidhi haja ya mazungumzo yao. Kwa hivyo, tafiti hizo zilikuwa ni dira na muelekeo wa kazi hii katika kukamilisha malengo yake.

Mohammed (2013) alifanya utafiti juu matazamo wa wanafunzi na walimu kuhusu matumizi ya lugha tandawazi katika Kiswahili. Matokeo ya kazi hii ni kuwa sababu za kutumia lugha tandawazi ni kuokoa muda, kupunguza gharama, kufupisha maandishi na kupata urahisi wa kuandika. Kwa upande wa athari za lugha tandawazi zipo athari za kiisimu na athari zisizo za kiisimu. Miiongoni mwa athari za kiisimu ni

athari katika fonolojia, mofolojia na kisemantiki. Maelezo haya yanaonesha ni kwa kiasi gani na kwa vipi lugha huweza kuathirika. Ila kazi hii imejikita zaidi katika matumizi ya lugha ya maandishi katika simu za mikononi. Rejeleo hii inaendana na tafiti tangulizi zilizofanyika katika maeneo mbali mbali kuhusu lugha tandawazi kama vile; Angel (2004) aliyefanya utafiti wa ujumbe wa simu za kiganjani kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Hong Kong akiangalia jinsia katika mawasiliano ya lugha mbili.<sup>1</sup> Lengo kuu la utafiti huo lilikuwa ni kupata taarifa juu ya nani hasa wanaotumia ujumbe mfupi, kwa kasi gani, wanawatumia nani, kwa lengo gani na kwa kutumia lugha gani. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa jinsia ya kike ndio inayotumia zaidi mawasiliano kwa njia ya ujumbe mfupi. Njia hii huitumia kwa maamkizi na wakati wa kusalimiana katika sherehe mbalimbali kama vile krismas na sherehe za kuzaliwa. Ujumbe huo hutumwa kwenda kwa rafiki zao wa jinsia moja. Pia utumaji wa ujumbe mfupi wa simu za kiganjani hutumiwa zaidi na wanafunzi wakubwa kuliko wanafunzi wadogo na hutumia zaidi lugha ya Kiingereza wakati wanafunzi wadogo huchanganya na kubadili misimbo. Hii ni kwa sababu wanafunzi wakubwa ndio wenge umilisi wa Kiingereza. Vilevile idadi kubwa ya wanafunzi wakubwa hutumia ujumbe kuwasiliana na ndugu zao pamoja na wapenzi wao ukizingatia zaidi maudhui ya kimapenzi wakati wanafunzi wadogo hutuma ujumbe wenge maudhui ya kiutani zaidi.

Hali kadhalika, matokeo yalionesha kuwa watumiaji wakuu wa ujumbe wa simu hutuma ujumbe kwa lengo la kushajihisha ushirikiano wa kisiasa na kujenga mahusiano na rika lao hususani mahusiano ya kijamii. Ingawa utafiti wake ulilenga

---

<sup>1</sup><http://www.fibreiculture.org/jornal/issue6/issue6-lin.html>.

kutaka kujua ni nani hasa wanaotumia ujumbe mfupi na kwa lengo gani haukuweza kubainisha athari za msamiati katika lugha aliyoifanyia utafiti.

Stigand (1915) anaeleza kuwa alikuwa na lengo la kueneza msamiati mwingi wa lahaja, alifanya hivyo kwa hofu kwamba kadiri maendeleo ya lugha yanavyoendelea kukua, msamiati wa lahaja mbalimbali utapotea. Kwa hivyo, alianda kazi ambayo ilibeba msamiati mwingi wa lahaja katika maandishi na matamshi yake ili kuonesha uhalisia wa msamiati huo. Kutokana na msingi huo, aliorodhesha lahaja kumi na tano ili kuonesha utajiri wa lahaja na kuonesha wingi wa maneno na utajiri utakaoweza kukikuza zaidi Kiswahili. Utafiti huo ulizidisha ari ya ufanyakaji wa utafiti huu kwani, umemzindua mtafiti kuona utajiri uliopo katika Kiswahili na lahaja zake na kuonesha kuwa kuna haja ya kutosha katika kuzishughulikia lahaja za Kiswahili kwa maendeleo ya Kiswahili chenyewe.

Lihamba, (1981) anaonesha athari za kuenea kwa utamaduni wa jamii fulani na athari zake katika mabadiliko ya lugha au lahaja ya jamii hiyo, amesema kwamba binadamu huzaliwa na silika ya kuigiza sherehe, ngoma na vitendo vyta wahenga ambavyo ndivyo chanzo cha sanaa za maonesho. Mambo yote hayo huwasilishwa kwa kutumia lugha. Kwa mtazamo wake, vyanzo vyta sanaa za maonesho vilizaliwa na kuendelezwa kutokana na uchu wa binadamu wa kuangalia kwa makini ulimwengu wake, huiga matendo yake mwenyewe au kuyavumbua matendo hayo katika ujenzi wa dini na tamaduni zake. Alihitimisha maelezo yake kwa kudai kuwa wakati wote sanaa za maonesho hubakia kuwa ni kazi ya kufunza na kustarehesha kupitia lugha iliyotumika.

Kwa mujibu wa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa kila sehemu ya jamii huwa na aina yake ya utamaduni na maigizo ambayo huwatambulisha watu wa sehemu husika. Kwa mfano, katika kijiji cha Makunduchi kuna utamaduni wa ‘Mwaka Kogwa’ wanaouadhimisha kila mwaka mara moja. Huo ni utamaduni uliorithiwa na ambao huwatambulisha watu wake. Kinachoangaziwa katika utamaduni huo kwa kuhusisha na utafiti huu sio namna ya mwaka kogwa na uchezaji wake, bali ni lugha inayotumika katika sherehe hizo. Kiasili ni kuwa sherehe ziliwahusu Wamakunduchi wenyewe peke yao, kwa hivyo, lahaja ya Kimakunduchi ilizitawala sherehe hizo. Ama kwa sasa kwa kuwa sherehe zimetaifishwa na kuwa sherehe za Kitaifa, zimeondoa ile hadhi ya kutumia lahaja moja kwa moja ili kuwapa fursa waliohudhuria kufahamu kinachozungumzwa kwa nafasi yao. Kufanya hivyo imeleta athari kwa lahaja ya Kimakunduchi.

Kwa upande wa Kitala (2006) anaeleza kwamba, utamaduni uliopo katika lahaja una mchango ndani ya lugha ya Kiswahili. Uelewa mzuri wa utamaduni wa lugha husika huweza kuwasilishwa kwa kupitia lahaja katika mambo mbalimbali. Anaendelea kueleza kwamba lugha ili ikamilike ni lazima ijikite katika utamaduni wake, mambo mengi kama vile, maingiliano ya watu, sherehe za misiba na furaha, utumizi wa lugha na utani katika jamii husika, sherehe za kimila kama mwaka kogwa kwa Makunduchi, na shughuli nyingine zinazoandamana na utamaduni, huchochea utambulisho wa jamii na lugha katika utamaduni wa lugha husika. Maelezo haya yanakazia uelewa wetu kwamba kama katika lugha ndimo mna utamaduni wa jamii husika basi ni vigumu utamaduni huu kujificha pale mzungumzaji wa lugha hiyo anapozungumza lugha ama lahaja nyingine tofauti na ile ya kwake. Kimakunduchi

kina utamaduni wake kama zilivyo lugha ama lahaja nyingine za lugha ya Kiswahili jambo ambalo linafanya mzungumzaji wa Kimakunduchi kudhihirisha utamaduni huo pale anapozungumza Kiswahili Sanifu. Swali linabaki kuwa, kutokana na muingiliano wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi, kunatoa athari gani kwa lahaja hiyo na utamaduni wake?

Maelezo ya hapo juu yametoa muelekeo wa ufahamu wa umuhimu wa lahaja na utamaduni wake. Kwa hivyo, maelezo hayo yalimuongoza mtafiti kubaini nafasi ya utamaduni na uhifadhi wa lahaja za Kiswahili kwa maendeleo ya Kiswahili chenyewe.

## **2.5 Mkabala wa Kinadharia /Kiunzi cha Nadharia**

Kadiri ya Masamba (2009), nadharia ni taratibu kanuni na msingi uliojengwa kwa mawazo kwa madhumuni ya kuwa kigezo cha kuelezea jambo au mambo kadhaa. Utafiti huu ulitumia nadharia ya mwathiriano wa lugha ili kuweza kukusanya na kuchambua data za utafiti. Ukusanyaji na uchambuzi huo uliongoza katika kufikia utoaji wa matokeo ya utafiti huu. Nadharia hiyo imekuwa ni faafu na imesaidia kupatikana kwa ukamilifu lengo la utafiti.

Nadharia ya mwathiriano wa lugha ni nadharia ambayo inachunguza kwa makini ukaribu na muingiliano wa lugha ulivyo katika jamii husika. Mwathiriano wa lugha ni matokeo ya mabadiliko ya kiisimu yanayoweza kutokea kati ya lugha inayoathiri na inayoathiriwa. Mabadiliko hayo hutokea kutokana na mawasiliano ya karibu kati ya wanajamii wa lugha zinazozungumzwa (Thomason, 2001:62). Fasili hii inashughulikia mabadiliko yote ya kilugha ambayo huifanya lugha moja kuiathiri

lugha au lahaja nyengine kwa kuhamishia misamiati na dhana nyengine za lugha, yaani kesi zote za kiisimu kuingiliwa, na pia inajumuisha mabadiliko mengine yanayohusiana na lugha hiyo. Mwingiliano wa lugha ama lahaja huwa na athari za kimawasiliano kati yao na kusababisha lugha au lahaja moja kuikalia juu lahaja nyengine. Athari hizo za mawasiliano huweza kujitokeza katika mambo yafuatayo: Kwanza, mabadiliko ya mwathiriano hutokea taratibu na yanaweza kusababisha kuiua lugha au lahaja moja, hasa kama lahaja hiyo itakuwa na udhaifu ama wa watumizi au mawanda ya msamiati. Ama lugha itakayochukuwa nafasi baada ya kufa kwa lugha ya kwanza haitokuwa sawa na ile lugha au lahaja iliyokufa katika hali zote.

Pili ni kuwa, lugha au lahaja iliyio karibu na lahaja ambayo inapokea mabadiliko ndiyo ambayo ina nafasi zaidi ya kuiathiri lahaja hiyo kutokana na ukaribu wa watu wake na mawasiliano ya jamii hizo.

Tatu ni kuwa, kuna mabadiliko mengine hutokea kwa njia isiyotarajiwa yaani si ya moja kwa moja, mabadiliko hayo hutokana na mwingiliano wa watu katika shughuli zao. Inaaminika kuwa mabadiliko ya kiisimu, msamiati na muundo wa lugha unaoingizwa taratibu katika lahaja inayochukuwa mabadiliko kutokana na mwathiriko huo, lahaja hiyo taratibu huanza kubadilika muundo wake na mtindo wa utumizi wa lugha kijumla.

Kwa jumla ni kwamba, wataalamu wa sarufi wanaamini kuwa mwingiliano wa lugha umekuwa na athari kubwa ya mabadiliko yanayoweza kuikumba lahaja moja katika

hali zake zote za kilugha kama vile; kuathirika kimsamiati, maana, lafudhi na mjengeko wa muundo wa lugha kijumla. Meillet (1921) kwa mfano anaamini kuwa ni lazima kuwe na uwiano kati ya lugha ambayo inakopa muundo wa lugha na ile ambayo inatoa muundo huo. Jakobson (1962 [1938]:241) anaeleza kuwa lugha (lahaja) inachukuwa mabadiliko iwapo lugha hizo (inayochukuwa mabadiliko na ile inayoiathiri nyengine) zikiwa na ukaribu na ukuaji wa maendeleo unaofanana.

### **2.5.1 Misingi ya Nadharia za Utafiti**

Nadharia iliyotajwa hapo juu, imetoa misingi ambayo imesaidia katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Misingi hiyo ni kama ifuatavyo:

- i) Lugha au lahaja zenyewe uwiano na ukaribu wa kilugha zina uwezekano mkubwa wa kuathiriana kimsamiati, maana, lafudhi na mjengeko wa muundo wa lugha kijumla. Matokeo hayo hujitokeza zaidi kwa lugha au lahaja inayothiriwa kupoteza msamiati wake na kuchukuwa msamiati wa lahaja iliyoizidi nguvu na mawanda ya utumizi.
- ii) Lugha au lahaja zilizo karibu ndizo ambazo zina uwezekano mkubwa zaidi wa kuathiriana. Mwathiriko huo pia unazingatia ukuaji wa maendeleo unaofanana.
- iii) Mwingiliano wa lugha au lahaja unaweza kuidhoofisha au kuiua lahaja moja. Lahaja inayothirika kwa kiasi kikubwa inakuwa hatarini kupoteza uhalisia na kusababisha kudhoofika na pengine kufa.

### **2.6 Pengo la Utafiti**

Kuna tafiti nyingi zilizozungumzia vipengele vya lugha na katika masuala la utandawazi katika lugha ni za jamii mbali mbali. Watafiti wengi walijikita katika

kutafiti athari ya uandishi wa ujumbe mfupi wa maandishi katika simu, dhana hii inaitwa lughatandawazi. Lughatandawazi ni sehemu ya athari za utandawazi katika lugha. Licha ya kuwa athari za sayansi na teknolojia zimeanza kutafitiwa tokea mwaka 2001 katika maeneo tofauti, tafiti hizo bado hazijatosheleza kwani kuna maeneo mengi yanahitaji kufanyiwa utafiti. Maandiko yaliyochambuliwa yanaonesha mapengo yafuatayo:- Kwanza, tafiti nyingi hazijajikita katika lugha ya Kiswahili na lahaja zake. Pili, katika baadhi ya tafiti zilizojikita katika lugha ya Kiswahili na lahaja zake kama vile Ali (2016) aliyetafiti juu ya athari ya kiutandawazi katika lahaja ya Kitumbatu, hakuweza kuchambua athari ya utandawazi huo katika kipengele cha kimsamiati. Tatu, lahaja ya Kimakunduchi ni mionganini mwa lahaja za Zanzibar zilizopata umaarufu mkubwa kutokana na utamaduni wa “Mwaka Kogwa” na kukua kwa suala la mawasiliano. Hali hii ilitosha kumfanya mtafiti kuona haja ya kuangalia athari iliyotokana mwingiliano na lahaja za karibu kama Kiunguja mjini ambacho kwa sasa ni Kiswahili sanifu kilivyoithiri lahaja ya Kimakunduchi kimsamiati na muundo wa lugha kijumla. Kutokana na hali hiyo, Mtafiti ameona kuna haja ya kutafiti athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kwa lengo la kuziba mapengo hayo.

### **2.6.1 Muhtasari wa Sura**

Sura ya pili ni kwa ajili ya kuwasilisha kazi tangulizi pamoja na kubainisha kiunzi cha nadharia. Kupitia eneo hili, dhana mbali mbali zinazohusu mada ya utafiti zilielezwa. Kwa jumla sura hii imejumuisha dhana ya msamiati ulioibuka kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi, msamiati ulioachwa kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya

Kimakunduchi na athari za Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi, nadharia ya utafiti pamoja na pengo lililojitokeza katika maandiko yaliyochambuliwa.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii imeelezea utafiti ulivyofanyika. Sura imeeleza eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya na kuchambulia data, udhibiti wa mbinu hizo, vifaa vilivytumika pamoja na changamoto zitakazojitokeza wakati wa kukusanya data.

#### **3.2 Mpango wa Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika uwandani na maktabani. Mwelekeo wa utafiti ni wa kifafanuzi (maelezo) na haukuhusisha taarifa za kitakwimu. Mtafiti alikwenda uwandani kuchunguza na kupata vielelezo kwa kuwahoji na kuwasaili wanajamii wa eneo la Makunduchi, wakiwemo wasomi ambao ni wanafunzi na walimu, (hasa wanaofundisha somo la Kiswahili), vijana pamoja na wazee. Utafiti ultumia dodoso kwa wasomi, mbinu ya uchunguzi wa kushuhudia na mahojiano kwa wazee na baadhi ya wasomi ambao ni wanafunzi wa shule za sekondari. Hatimaye mbinu ya mjadala ilijojumuisha vijana. Mbinu zote hizi zilitumika kwa lengo la kupata data za kiufafanuzi. Mbinu hii ilikuwa ni muwafaka katika uchambuzi na uwasilishaji wa data hizi kutokana na mada ya utafiti huu kutaka kujua athari ya maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi. Pamoja na mbinu hii, mbinu ya kiidadi ilitumika hususan katika kuchambua idadi ya sampuli iliyotumika katika utafiti huu. Kwa kiasi fulani utafiti huu ultumia mchanganyiko wa mbinu ya kiufafanuzi na kiidadi.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo lililofanyiwa utafiti huu ni mkoa wa Kusini katika wilaya ya Kusini, Zanzibar. Hii ni Wilaya mojawapo kati ya wilaya 10 za Zanzibar kama ilivyobainishwa na Mlacha na Hurskainen (1995). Wilaya hii inapakana na wilaya ya Kati kwa upande magharibi na bahari ya Hindi kwa upande wa mashariki. Eneo hili limegawika katika kanda tatu (3) ambazo ni Makunduchi, Pwani na Juu.

Kanda ya Makunduchi inajumuisha vijiji vya Mtende na Makunduchi ambapo ndipo makao makuu ya wilaya ya Kusini. Kanda ya juu ipo magharibi ya kanda ya Makunduchi, Kanda hii inaundwa na vijiji vya Kibuteni, Kizimkazi mkunguni, Kizimkazi dimbani, Muyuni, Muungoni, Kitogani, Pete na Jozani. Kanda ya Pwani ilioko upande wa kaskazini ya kanda ya Makunduchi. Kanda hii inajumuisha vijiji vya Bwejuu, Paje na Jambiani. Kwa mujibu wa sensa ya idadi ya watu ilifanyika Zanzibar mwaka 1998 eneo la Makunduchi lina wakaazi wapatao 31,853. Wamakunduchi hawa wametapaka kwenye eneo la kilomita za mraba zipatazo 361.2, pamoja na eneo hilo, mtafiti alitumia vyuo vikuu kama vile; Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Zanzibar vilioko Tunguu katika mkoa wa kusini Unguja. Ufafanuzi zaidi wa maelezo hayo umetolewa katika ramani iliyowasilishwa hapo chini.

Utafiti huu ulijikita zaidi na eneo la Makunduchi, eneo ambalo lina shehia ya Mzuri, shehia ya Nganani, shehia ya Kajengwa, shehia ya Kiongoni na shehia ya Tasani. Maeneo haya yamechaguliwa kutokana na kuwa na historia kubwa ya kutumia lahaja

hii, na hivi sasa kuonekana kuathirika hatua kwa hatua katika matumizi ya lajaja hiyo.



**Kielelezo 3.1: Ramani ya Kisiwa cha Unguja Inayoonesha Eneo la Utafiti**

Chanzo: Utafiti, 2018

### 3.4 Jamii ya Watafitiwa

#### 3.4.1 Kundilengwa

Kwa mujibu wa Williman (2001), kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanya utafiti. Hujumuisha watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao mtafiti ameamua

kuwatumia katika utafiti wake kwa lengo la kuweza kupata taarifa zitakazomsaidia katika kufikia malengo yake aliojiwekea. Katika utafiti huu kundi lengwa liliwahusisha vijana, wazee, pamoja na wasomi.

Mtafiti ameamua kutumia sampuli ya vijana wenyе umri kati ya miaka 18 hadi 30 wanaoishi Makunduchi kwa sababu vijana ndio wakwanza kupenda kupokea mabadiliko. Hivyo, mtafiti alipata fursa ya kuchunguza kwa kiasi gani msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi ilivyoathirika na kutokana na mwingilio wa Kiswahili sanifu. Kundi la pili ni wazee wanaoishi Makunduchi wenyе umri kati ya miaka 50 na kuendelea. Mtafiti alichagua sampuli ya wazee kwa kuwa wazee ndio waendelezaji na wazungumzaji wakuu wa lahaja hii ya Kimakunduchi. Lengo la kuchagua wazee ni kutaka kuchunguza kama bado wazee wanaendeleza kutumia misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi au tayari weshaaathirika na mwnigiliano uliotokana na Kiswahili sanifu. Kwa upande wa wasomi; utafiti umetumia walimu hasa wanaofundisha lugha ya Kiswahili na wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne.

### **3.5 Sampuli na Usampulishaji**

#### **3.5.1 Sampuli ya Utafiti**

Kothari (2004) anafafanua kwamba sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwayo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake. Utafiti huu ulihuisha sampuli ya watu 90 kati yao walikuwa wazee, vijana, na wasomi, hususan wanaotumia lahaja ya Kimakunduchi wakihuisha wanawake na wanaume. Mtafiti alichagua wazee wenyе uelewa wa masuala ya lahaja ya Kimakunduchi na historia yake kwa kuongozwa na Sheha wa

shehia husika pamoja na watendaji wa shehia hizo katika masuala ya mila na utamaduni. Mtafiti alichagua wasomi wa Kiswahili ambao pia ni wenyiji wa maeneo husika. Wasomi hao walikuwa katika makundi mawili makuu, kundi la kwanza ni wanafunzi wa skuli za sekondari za Makunduchi ili kubaini matumizi ya lugha na hali ya msamiati na mabadiliko yake. Kundi la pili wa walimu wa Skuli za Makunduchi ambao pia ni wenyiji katika jamii hiyo. Sampuli ya vijana imechaguliwa kutokana na kuwa wepesi wa kuathirika katika masuala ya lugha na utamaduni. Mtafiti alipitia sampuli 90 ambao ni moja ya kumi ya jumla ya walengwa 900 kama ni jumla ya walengwa waliokusudiwa kuwakilisha jamii ya Makunduchi.

Mgawanyiko wa sampuli hiyo ulikuwa kama hivi vifuatavyo :

### **Jedwali 3.1: Mgawanyiko wa Sampuli ya Watafitiwa**

<b>Sampuli</b>	<b>Idadi</b>	<b>Asilimia</b>
Wazee	25	27.77
Vijana	40	44.44
Wasomi	25	27.77
<b>Jumla</b>	<b>90</b>	<b>100</b>

Chanzo: Utafiti, 2018

### **3.5.2 Usampulishaji**

Kadiri ia Singh (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa ambayo sampuli hupata usampulishaji nasibu, na usio nasibu (usampulishaji usio nasibu). Usampulishaji nasibu ni mchakato wa kuchagua ambapo uwezekano wa kuchagua memba yoyote katika kundi lengwa hufanyika. Kwa upande mwingine tunaweza

kusema kuwa usampulishaji nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo kila memba katika sampuli ana haki sawa na mwensiwe katika kuchaguliwa. Usampulishaji usio nasibu ni mchakato wa kuteua sampuli ambapo mtafiti ana fursa ya kuteua nani amtumie katika utafiti wake na nani amuache na hatimaye kutoa matokaeo ya jumuishi wa watafitiwa wate. Mtafiti alitumia usampulishaji wa unasibu na usampulishaji lengwa. Alitumia usampulishaji wa unasibu kwa lengo la kupata data zilizowashirikisha watafitiwa wote na kuweza kufikia katika malengo. Malengo yaliyohusiana na msamiati yalihusisha zaidi wazee na vijana kutokana na kuwa wazee ndio ambao wana utambuzi wa msamiati wa asili wa Kimakunduchi na wanafahamu athari zinazojitokeza. Vilevile liliwahusisha vijana ambao ndio walioathirika katika matumizi ya msamiati ulio tofauti na ule uliokuwa ukitumiwa na wazee. Maana ya maneno yalitumika tofauti na yalivyokuwa yaktumika kabla. Lengo la pili ni kubainisha msamiati ulioongezeka katika lahaja ya Kimakunduchi kutokana na mwngiliano na Kiswahili sanifu. Katika kufanikisha lengo hili, wasomi, vijana na wazee walikuwa na nafasi kubwa ya ushiriki. Watafitiwa hao waliwezesha ukusanyaji wa data na uchambuzi wake na kupatikana matokeo ya utafiti. Lengo la tatu lilikuwa ni kutathmini athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi, ulioainisha mrengo wa mabadiliko ya msamiati kutokana na athari ya mwingilio wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi. Mtafiti aliweza kupata tathmini ya matokeo kutokana na muongozo wa lengo la kwanza na la pili ambayo yalishirikisha sampuli zote za watafitiwa wa utafiti huu. Watafitiwa wote hao walisaidia kupata maoni ya mustakbali wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na mabadiliko makubwa yanayojitokeza kutokana na athari za Kiswahili sanifu kilivyoweza kuiathiri lahaja ya Kimakunduchi. Vilevile usampulishaji huo wa kundi

lengwa ulimsaidia mtafiti kupata data za uhakika na zenyenye kuaminika na kumuwezesha kufikia kwa urahisi malengo yake.

### **3.6 Mbinu za Utafiti**

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu ni jumla ya njia zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu hizo zinawezwa kugawia katika makundi mawili ambazo ni mbinu za kukusanya data na mbinu za kuchanganua data. Kwa mujibu wa Kothari (keshatajwa) mbinu za kukusanya data ni njia mbali mbali ambazo mtafitia anazitumia ili kupata data zinazohitajika katika utafiti wake. Utafiti huu utatumia mbinu za aina tatu kama ifuatavyo.

#### **3.6.1 Mahojiano**

Kombo na Trmp (2006) wanaeleza kuwa mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au ya simu, barua pepe na kadhalika yaliofanyika kati ya watu wawili au zaidi. Williman (2001) amechambua mahojiano kwa kuyagawa mahojiano haya katika aina tatu. Kwanza ni mahojiano ya ana kwa ana. Pili, ni mahojiano ya kundi na, tatu ni mahojiano ya simu (mtandao). Kwa upande wa Kothari (2004), anaeleza kuwa mahojiana ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti huwa uliza maswali watafitiwa wake na wakati mwengine mtafitiwa hupata fursa ya kumuuliza maswali mtafiti. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa wanajamii wa Makunduchi ambao ni vijana na wazee. Lengo la kutumia mbinu hii ni kuweza kupata data zilizohusiana na mabadiliko ya msamiati kimaana kutokana na athari ya Kiswahili sanifu ilivyoathiri lahaja ya Kimakunduchi na msamiati ulioongezeka au kutumika kwa mbadala na ule uliopo katika lahaja ya Kimakunduchi kutokana na mwingiliano na Kiswahili sanifu.

Mbinu hii pia ilirahisha kupata data za kina na kwa urahisi kutoakana na kupata fursa ya kuwahoji sampuli ambao wengi wao kwa upande wa wazee hawawezi kusoma. Mtafiti alitumia mbinu hii ili kupata urahisi wa kupata data kwa watu wasiojua kusoma kama vile wazee na wajina wasiokwenda shule.

### **3.4.1 Mjadala wa vikundi**

Hii ni mbinu ambayo ilijumuisha watu wengi kwa wakati mmoja wakijadili kwa pamoja dhana fulani iliyowasilishwa. Mtafiti aliitumia mbinu hii ili kupata kubaini ukinzani unaoweza kujitokeza kuhusiana na mitazamo ya watu mbalimbali kuhusiana na athari za Kiswahili sanifu kwa msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi wakiwa pamoja. Katika mbinu hii vikundi vitatu vilivyojumuisha vijana, wazee na wasomi. Kila kikundi kilihushisha watu tisa; wazee watatu, vijana watatu na wasomi watatu. Mbinu hii ilisaidia kuibua mitazamo mbalimbali iliyofanikisha upatikanaji wa data za utafiti huu.

Mbinu na zana zilizotumika katika kukusanya data ziliteuliwa kutokana na kiini cha utafiti huu kuhusisha watafitiwa wenyе tofauti katika viwango vya kielimu, upeo wa kifikra, uzoefu wao katika matumizi ya msamiati wa Kimakunduchi na umri wa watafitiwa ambao umewezesha kupata maelezo ya mabadiliko ya msamiati wa Kimakunduchi. Njia hii imetumika kwa lengo la kukutanisha watu wenyе umri tofauti na mtazamo tofauti katika jamii ili kupata mitazamo yao juu ya mabadiliko ya lahaja hiyo.

### **3.4.2 Ushuhudiaji**

Bakari (2015) anaeleza kuwa ushuhudiaji ni mbinu ya kukusanya data inayohusiana na kurikodi data za watu, vitu na matukio katika mpangilio maalumu. Mbinu hii ilitumika kwa lengo la kupata data zilizomsaidia mtafiti katika kufikia lengo lake la kwanza ambalo ni kubainisha njia zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu. Mtafiti alikwenda mwenyewe uwandani ili kushuhudia namna Wamakunduchi wanavyozungumza msamiati wa lahaja yao na kuchunguza kwa kiasi gani msamiati huo umeathirika kutokana na muingiliano wa Kiswahili sanifu. Maeneo yaliyoshuhudiwa ni katika shughuli za harusi, kwa kulinganisha harusi za Wamakunduchi walizofanyia Makunduchi na zile walizofanyia maeneo ya Mjini wa Unguja. Mtafiti alishuhudia lugha inayotumika katika ufundishaji katika skuli mbalimbali za jamii ya Makundchi. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data zenye kuaminika na kupunguza dosari kwa kuwa mtafiti mwenyewe alishuhudia na kuona hali halisi ya athari ya Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi. Njia hii imetumika kwa lengo la kulinganisha matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi inavyoweza kutumika katika mazingira tofauti kwa wanajamii hao.

### **3.4.3 Hojaji**

Kothari (2004) anelaza kuwa hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha huyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti. Williman (2001) naye anaeleza kuwa maswali ya hojaji yapo ya aina mbili, aina ya kwanza ni maswali fungo ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jibu mionganoni mwa majibu kadhaa yaliyopendekezwa. Aina hii ni rahisi

kwa watafitiwa kutoa majibu na inaepusha upendeleo pia inasaidia kutoa majibu mahsus. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni yale yanayohusisha maswali ya wazi. Maswali haya mtafitiwa hupata fursa ya kueleza anachokijua juu ya kile alichoulizwa. Mtafitiwa hupata fursa ya kutoa mawazo yake kwa uwazi na ubainifu na mtafiti kupata taarifa nyingi zaidi. Mtafiti ameamua kuchagua mbinu hii kutokana na faida mbali mbali zilizotajwa na wataalamu mbali mbali. Wataalamu hao ni, Enon (1998), Woods (2001) na Mulokozi (1983) wanassema kuwa hojaji zinaweza kuwahoji watafitiwa wengi kwa wakati mmoja pia zinaweza kuibua taarifa nyingi kwa muda mfupi. Maswali ya hojaji huwa sawa kwa watafitiwa wote. Mtafiti alitumia maswali fungo na maswali ya wazi ili kupata taarifa za kina kutoka kwa sampuli ya utafiti huu. Mtafiti alitumia sampuli inayohusiana na wasomi ambao ni wanafuni na walimu katika jamii ya Makunduchi. Mbinu hii ilitusaidia kutathmini mrengo wa msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano na Kiswahili sanifu. Pia, mbinu hii imeteuliwa na kutumika kwa wasomi ili kuwapa fursa na wakati kwa watafitiwa kufikiria kwa kina jawabu za maswali waliyoulizwa.

### **3.5 Usanifu wa Utafiti**

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unaotoa mchoro kamili juu ya namna au jinsi utafiti fulani utakavyofanyika tangu hatua za mwanzo kabisa hadi kamilika kwake (Babbie 1999). Zipo aina mbali mbali za usanifu wa utafiti na kulingana na utafiti huu. Mtafiti alitumia uchunguzi kifani kuwa aina ya usanifu huu. Uchunguzi kifani ni aina ya uchunguzi ambapo mtafiti huteua sehemu tu ya watafitiwa au vitafitiwa vilivyo vingi kwa lengo la kufanya utafiti ambapo bila ya shaka vilitoa uwakilishi wa watafitiwa au vitafitiwa vyote. Katika utafiti huu, mtafiti aliteua

maeneo ya Mzuri, Kiungoni Nganani, Kajengwa na Tasani. Mtafiti aliamua kuteua maeneo haya kutokana na kuwa maeneo haya yana wazungumzaji wa asili wa lahaja ya Kimakunduchi. Kothari (2009) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni aina bora ya usanifu kwa sababu utamfanya mtafiti kutumia muda mfupi na gharama nafuu kupata data za utafiti na kukamilika malengo yake.

### **3.6 Mbinu za Kuchambua Data**

Data katika utafiti huu zilichambuliwa na kufafanuliwa kwa kipitia mkabala wa kimaelezo (kiufafanuzi) pamoja na takwimu. Enon (1998). Anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kueleza na kufafanua data ambazo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Krees (2008) anaeleza kuwa mkabala huu unaeleza vipi na kwa nini matukio yametokezea, kutokana na maumbile ya kazi yake. Hivyo, kutokana na maumbile ya utafiti huu, mtafiti alitumia mikabala miwili, yaani wa kimaelezo na wa kitakwimu ili kuweza kupata data na uchambuzi ambao ulionesha ni kwa kiasi gani na vipi matokeo ya utafiti yalijitokeza katika ukusanyaji na uchambuzi wake.

### **3.7 Muhtasari ya Sura**

Maeneo yalioelezwa katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji pamoja na mbinu za kukusanya data na uchambuzi wake. Mbinu kuu ambazo mtafiti alizitumia ni mbinu ya mahojiano, mbinu ya hojaji, mijadala ya vikundi na mbinu ya ushuhudiaji pamoja na usanifu wa utafiti na mbinu za kuchambua na kufafanua data pia zimeelezwa katika sura hii.

## SURA YA NNE

### **4.0 UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura hii, utafiti umewasilisha, kunyambua na kujadili data mbalimbali zilizokusanywa wakati wa utafiti kutoka katika maeneo yaliyoteuliwa, ikiwa ni pamoja na data za maktabani. Mjadala juu ya uchambuzi wa utafiti ulifanywa kuhusu athari zilizosababishwa na mwingilio wa Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi.

Sehemu hii imegawanywa katika sehemu kuu tatu zilizoakisi malengo na maswali yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza imebainisha njia zinazotumika katika kuiathiri lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja hiyo. Sehemu ya pili, imebainisha msamiati ulioachwa na ulioibuka kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi na sehemu ya tatu imetathmini athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na athari ya mwingiliano wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Vile vile sura hii imeonesha uwasilishaji, mjadala, uchanganuzi na matokeo ya utafiti huu kutokana na data zilizokusanywa kuhusiana na athari za mwingiliano wa Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi.

Mwisho wa sura hii, mtafiti ametoa muhtasari kwa kudondo mambo yote yaliyojadiliwa katika sura hii ambayo ndiyo matokeo ya utafiti wenywewe.

## **4.2 Njia Zinazotumika Kuathiri Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi Kutokana na Maingiliano ya Kiswahili Sanifu**

Katika kufanikisha lengo mahsusini la kwanza la utafiti, mbinu tofauti zilitumika. Mtafiti aliwahoji wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na wanafunzi wa Chuo Kikuu Zanzibar ambao ni wenyeji wa Makunduchi juu ya njia zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi uliotokana na mwingiliano wa Kiswahili sanifu. Kisha mtafiti aliwataka waorodheshe njia na mfano wa msamiati huo na kuuonesha ni katika nyanja zipi za kimaisha lahaja hiyo inaathiriwa.

Pamoja na kundi hilo lililotajwa la watafitiwa, mtafiti pia alipata nafasi ya kuingia Makunduchi na kuzungumza na wakaazi wa Makunduchi. Katika mbinu hiyo kulitumika zana kama vile hojaji, mahojiano na ushuhudiaji. Njia hizo zilitumika ili kupata data zilizosawa na watumizi halisi wa eneo husika.

Matokeo ya lengo hili yalikusanywa kwa kupitia mahojiano, hojaji na udurusu wa maktabani. Mahojiano hayo yalionesha kuwa kuna mabadiliko ya msamiati wa lahaja ya Kimakundichi iliyotokana na ubadilikaji wa matumizi yake. Data zote hizo zilichambuliwa kwa kutumia nadharia ya mwathiriano wa lugha. Matokeo ya lengo hili yalijibainisha kutokana na mwingiliano wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi katika nyanja zifuatazo:

### **4.2.1 Mwingiliano Kuptia Vyombo vyaa Habari**

Vyombo vyaa habari vinachukuwa nafasi kubwa ya uenezaji wa taarifa mbalimbali katika jamii zote, kwa hivyo athari zake zinaweza kuwa ni kubwa kutokana na

mahitaji ya jamii kutaka kupata taarifa ya kinachoendelea katika habari za ndani na nje ya nchi. Utafiti umebaini kuwa vyombo vya habari ni njia kubwa inayotumika katika mawasiliano. Na kwa sababu vyombo hivi hutumia lugha sanifu, hivyo vimekuwa na nafasi kubwa ya kuathiri lahaja nyingine kama vile Kimakunduchi. Njia hii ni mionganini mwa njia kuu ambazo hutumika katika kuathiri lahaja nyingine kama inavyoeleza nadharia ya mwathiriano wa lugha kama inavyoeleza kuwa mabadiliko mengine hutokea kwa njia isiyotarajiwa yaani si ya moja kwa moja mabadiliko hayo hutokana na mwingiliano wa watu katika shughuli zao. Hii ni kwa kuwa vyombo vya habari vimekuwa vikiwakaribisha watu wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu na hivyo Kimakunduchi kuathiriwa moja kwa moja na Kiswahili.

Kwa mfano katika habari za michezo kuna neno “dafya” lenye maana ya “pata” lilitumika katika Kimakunduchi cha asili kuashiria ushindi. Kwa mfano, katika sentensi “Timu ya Santosi idafyu goli moja jana” likiwa na maana kuwa timu ya Santosi imepata goli moja jana. Kutokana na vyombo vya habari wanavyotumia Wamakunduchi kutumia sana neno “pata” neno hili limekuwa maarufu na kuanza kutumika katika lahaja hii. Maneno mengine ambayo yamekuwa maarufu sana katika vyombo vya habari na kuibuka katika kuchukuwa nafasi kubwa ya matumizi katika lahaja ya Kimakunduchi au kutumika sambamba yakiwa na maana ileile ni kama vile; “chochea, vitisho, chelewesha na kubaka”.

Kwa hivyo, vyombo vya habari vimekuwa ni nyezo ya maingiliano ya kilugha na kuathiri jamii katika matumizi ya lugha hizo, hivyo kusababisha jamii fulani ya

lahaja kukua au kudumaa kutokana na kuongeza au kupoteza msamiati wake. Maelezo haya yanatiwa nguvu na Mjawiri, (2016) ambae anaeleza kuwa vyombo vy'a habari kama ni sehemu ya utandawazi kwani ndivyo vilivyokuza msamiati, istilahi na mitindo ya lugha ya Kiswahili na kuifanya lugha hii ivume, inawiri, na itambulike duniani kote.

#### **4.2.2 Mwingiliano Kupitia Elimu**

Kiswahili sanifu ndio lahaja ambayo inatumika katika shughuli zote rasmi kama alivyobaini Maganga (1997) kuwa Kiswahili Sanifu kilichofanywa na wa kamati ya usanifishaji lugha ya Kiswahili ndicho kilichokubalika na serikali na kutumika katika shughuli rasmi kama vile elimu, utawala, mahakama na katika mikutano ya hadhara. Kwa hivyo, Kiswahili sanifu kimekuwa na nafasi ya kuziingilia na kuziathiri lahaja hasa za hapa Zanzibar kwa wepesi zaidi.

Utafiti umebaini kuwa, walimu na wanafunzi wakiwa katika shule zao, hupaswa kutumia Kiswahili sanifu kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Matokeo yake ni kuwa watoto huathirika taratibu na msamiati ambao wanautumia wakiwa shule na kuanza kuutumia pia wakiwa katika mazingira yao ya kawaida. Kuna maneno ambayo hutumika katika uwanja huu wa elimu ambayo huwfanya walimu waujengee mazowea na kuutumia pamoja na kuwa si msamiati wa asili wa Makunduchi. Hali hii imethibitika kutokana na asilimia sitini na mbili ya sampuli wasomi ambao ni sawa na wasomi ishirini na tatu (23) kati ya sampuli ya wasomi ishirini na tano (25) wamekuwa wakitumia Kiswahili sanifu badala ya kutumia lahaja ya Kimakunduchi pale walipokuwa wakizungumza na mtafiti wa kazi hii.

Elimu imekuwa ni njia kubwa ya kuathiri lahaja ya Kimakunduchi kutokana na jamii kubwa kuathirika na msamiati wa Kiswahili sanifu unaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wanapokuwa mashulenii. Hii ni kwa sababu, wanafunzi hao hulazimika kusoma, kujifunza na kujibu mitihani yao kwa kutumia Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa, wanafunzi wa sekondari hujilazimisha kadiri wawezavyo kuhakikisha kuwa wanatumia Kiswahili sanifu katika kazi zao. Kwa kufanya hivyo, athari hiyo hubakia katika matumizi yao ya lugha wanayoitumia kila siku.

Mfano wa msamiati wa Kiswahili sanifu unaotumika badala au sambamba na ule wa Kimakunduchi katika uwanja wa elimu ni kama vile; “kuanguka, kufeli, kupasi, hodari, mtoro, mijadala, wanafunzi, walimu, vitabu, kufoji, kusaidia, n.k.” Hayo ni baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu yanayotumika katika lahaja ya Kimakunduchi.

#### **4.2.3 Mwingiliano Kupitia Utamaduni**

Lugha ni mionganii mwa vipengele vya utamaduni, kwa hivyo, kuathirika kwa utamaduni hutoa taathira pia kwa lugha husika. Hii ni kwa sababu utamaduni hugusia nyanja zote za kimaisha. Vlevile utamaduni hugusia rika na jinsia zote, na hutolewa na kurithishwa kwa kupitia lugha. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa utamaduni ni nguzo muhimu ya uhifadhi wa lugha na lugha ndio msingi wa utamaduni wowote ule (Ussi, 2010).

Kutokana na maelezo hayo hapo juu, inadhihirika kuwa athari ya mwingilio wa Kiswahili sanifu uliojiingiza katika utamaduni wa Kimakunduchi umeiathiri pia

lahaja yake. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa kuna msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi ulioathiriwa kutokana mwingiliano wa Kiswahili kupitia maswali ya kiutamaduni. Mwaka kogwa ni kitambulisho kikuu cha utamaduni wa Makunduchi. Data zilizokusanywa zilionesha kuwa kuifanya sherehe ya mwaka kogwa kuwa na sura ya kitaifa kumetoa nafasi kwa Kiswahili sanifu kuingiza msamiati mwingi katika Kimakunduchi kwa sababu viongozi wanaohudhuria katika sherehe hizo hawakijui Kimakunduchi na inakuwa vigumu kufahamu baadhi ya vipengele hivyo. Mfano, neno “Nairuzi” neno hili lilikuwa likitumika badala ya neno “Mwaka Kogwa”. Kwa hivyo Kiswahili sanifu hutumika ili kuwasaidia viongozi kufahamu yanayozungumzwa katika sherehe hizo. Maelezo haya yanatiliwa nguvu na msingi wa nadharia ya mwathiriano wa lugha unaoeleza kuwa; Mabadiliko mengine katika lugha hutokea kwa njia isiyotarajiwa, yaani si ya moja kwa moja. Mabadiliko hayo hutokana na mwingiliano wa watu katika katika shughuli zao.

#### **4.2.4 Mwingiliano Kupitia Biashara**

Wakaazi wa Makunduchi hawawezi kujitenga na kubaki peke yao katika shughuli zote za kimaisha. Wana mahitaji mengi yanayowafanya wachanganyike na watu wa sehemu mbalimbali. Kwa hivyo, huwapasa kufanyakazi na watu wa sehemu tofauti ili kukamilisha mahitaji yao. Mionganini mwa sehemu muhimu ya mahitaji hayo ni katika masoko ambayo kwa kiasi kikubwa yanatawaliwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu.

Utafiti umebaini kuwa, watu wa Wamakunduchi kuchanganyika na watu wa sehemu za mjini na maeneo mengine yanayotumia Kiswahili sanifu, wameathiriwa na namna

ya uzungumzaji wa sehemu hizo. Watumizi wa lahaja ya Kimakunduchi hupaswa kuzungumza Kiswahili sanifu kutokana na imani kuwa watu wa sehemu nyengine hawatoweza kuwafahamu. Hali hii ni kama ilivyoelezwa na Mohammed (2013) ambaye anasema kuwa licha ya kutambulika kuwa Kimakunduchi ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili, kuna utofauti mkubwa wa kimsamiati kati ya lahaja hiyo na lahaja sanifu. Akimnukuu Wakili, katika nukta hii anasema kuwa katika dibaji ya Msamiati wa Pekee wa Kikae ilioandikwa na Rais wa Nne wa Zanzibar, Mhe. Idris Abdul Wakil anasema: "...kwa sababu hiyo baadhi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili." Bila ya shaka, maneno hayo yalivyoelezwa, ndivyo ilivyo. Kukifahamu Kimakunduchi kwa mtu asiyé Mmakunduchi, ni shida mno. Hii inatokana na utofauti mkubwa uliopo kati ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi na lahaja sanifu ya Kiswahili.

Kutokana na maelezo hayo, Wamakunduchi huzungumza Kiswahili sanifu ili kurahisisha na kukamilisha mahitaji yao. Jambo hilo husababisha msamiati wa Kiswahili sanifu kuiathiri lahaja ya Kimakunduchi. Mfano, maneno kama kilo, nusu kilo, robo kilo yamekuwa yakitumika badala ya pishi, kibaba na ratili. Utafiti ulibaini kuwa vijana wa Makunduchi hawajui kabisa vipimo vyá pishi, kibaba na ratili. Misamiati hii imebakia kwa wazee na ni nadra kuitumia kutokana na kutokuwa na haja ya kutumika. Maelezo haya yanatiliwa nguvu na msingi wa nadharia ya mwathiriano wa lugha unaoeleza kuwa; Mabadiliko mengine katika lugha hutokea kwa njia isiyotarajiwa, yaani si ya moja kwa moja. Mabadiliko hayo hutokana na mwingiliano wa watu katika katika shughuli zao.

Hali inamaana kuwa maingiliano ya shughuli ya kibiashara katia ya jamii ya watumiaji wa Lahaja ya Kimakunduchi na ile ya watumiaji wa Kiswahili sanifu yamekuwa naa athari kwa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na Kiswahili sanifu kuwa na nguvu ya kutumika katika shughuli hizo, na kuwajengea mazowea wenyiji wa Makunduchi kutumia zaidi Kiswahili sanifu kuliko hata lahaja yao.

#### **4.2.5 Mwingiliano Katika Uhamiaji na Uhamaji**

Utafiti umebaini kuwa mionganini mwa njia zinazoathiri lahaja ya Kimakunduchi ni uhamiaji na uhamaji wa wanajamii kutoka Makunduchi kwenda mjini na kutoka mjini kwenda Makunduchi. Kutokea kwa uhamiaji kwa njia yoyote kati ya hizo zilizotajwa kunaathiri lahaja ya Kimakunduchi. Hii ni kwa sababu watu wanaohamia au wanaohama katika kijiji cha Makunduchi huhitaji kuwasiliana na wenyiji wao, kwa hivyo hutumia Kiswahili sanifu na kuwafanya wenyiji kuvutika na kuwasiliana na watu hao. Kwa wale waliohamia katika sehemu nyingine kama vile eneo la mjini Unguja, hupaswa kutumia Kiswahili sanifu kutokana na idadi kubwa ya watu ambao wanatumia lahaja hiyo. Swala la uhamaji na uhamiaji umekuwa ukiathiri misamiati katika nyanja na njia tofauti. Utafiti ulibaini kuwa nyanja hii imeathiri zaidi katika misamiati ya kijamii na kiutamaduni kutokana na misamiati mipywa wa Kiswahili sanifu kuathiri nyimbo za michezo ya watoto. Mfano wa nyimbo za michezo iliyoathriwa na hali hii ni pamoja na mchezo wa mchicha, Kitambaa cheupe na Kifanifani.

Tafsiri ya matokeo haya ni kuwa, mwingiliano wa Kiswahili sanifu umeathiri lahaja kwa kiwango kukibwa. Kwa sababu umejipenyeza katika sehemu muhimu ambayo

uambukizaji wake huwa ni wa milele. Matokeo ya hali hiyo ni kuwa, watoto hao wakifiki wakati wa ujana na uzee wao watakuwa na msamiati mchache sana wa asili katika lahaja ya Kimakunduchi wanaoutumia kikawaida katika mazungumzo yao ya kila siku.

#### **4.2.6 Mitandao ya Kijamii na Vyombo vyta Mawasiliano**

Kutokana na ukuaji mkubwa wa mawasiliano katika ulimwengu wa sasa, kumekuwa na athari pia za matumizi ya lugha. Kwa mfano katika lugha ya Kiswahili, matumizi ya Kiswahili sanifu huchukuwa nafasi kubwa zaidi. Hii ni kwa sababu mawasiliano hayo huhusisha watu wa sehemu na lahaja tofauti. Vyombo vyta mawasiliano vilivybainika na kufanyiwa kazi katika utafiti huu ni pamoja na usafiri wa barabarani, matumizi ya simu pamoja na mitandao ya kijamii.

Katika njia zote za mawasiliano zilizotajwa hapo juu, mtafiti alichunguza mwingiliano wa Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi. Ilibainika kuwa kuna njia hizi zimekuwa ni miuongoni mwa njia za kuathiri lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maneno ya Kiswahili sanifu ambayo yanatumika zaidi katika njia hizo kuliko yale ya asili ya Kimakunduchi. Mfano kuna maneno kama simu na mtandao ni maneno mapya katika lahaja ya Kimakunduchi. Barabara na Honda yanatumika badala ya Baraste na tututu. Mtafiti pia alichunguza sababu ya utumizi huo wa maneno na kubainika kuwa uenezi, mawanda ya matumizi na utofauti wa lahaja za wazungumzaji vilichangia kutumia Kiswahili sanifu badala ya Kimakunduchi.

Kipengele cha mawasiliano kimeonekana kuchukuwa nafasi kubwa zaidi ya kuathiri lahaja ya Kimakunduchi, kutokana na matmizi ya Kiswahili sanifu katika nyanja

hizi. Hii ni kwa sababu vyombo vya mawasiliano kama vile simu vinatumia na watu wengi hususan vijana na wasomi. Utafiti ulibaini kuwa asilimia mia ya sampuli ya vijana na wasomi waliohojiwa katika utafiti huu wanamiliki na kutumia simu. Kwa upande wa sampuli ya wazee ni asilimia mia wamesha wahi kutumia simu kwa ajili ya mawasiliano na watu mbalimbali. Watumiaji hao wa simu huwasiliana na watu wa sehemu mbalimbali ambao wanatumia lahaja tofauti. Kutokana na haja ya kuwa na mawasiliano ya kufahamiana, Kiswahili sanifu hutumika zaidi ya lahaja ya Kimakunduchi. Kwa hivyo, mtu atakaekuwa na mawasiliano na watu wengi huweza kuathirika na kuwaathiri wengine kutoka eneo hilo.

#### **4.3 Msamiati Usiotumika na Ulolioibuka Kutokana na Maingiliano ya Kiswahili Sanifu Katika Lahaja ya Kimakunduchi**

Lengo la pili la utafiti huu linaeleza kuwa “Kuchambua msamiati ulioachwa na ulolioibuka kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi. Katika kufanikisha lengo hili, mbinu tofauti zilitumika. Mtafiti aliwahoji wazee na vijana wa Makunduchi pamoja na wataalamu wanaojua lahaja ya Kimakunduchi. Katika mahojiano hayo, ilibainika kuwa kuna msamiati ambao umeibuka kutokana na mwiningiliano na Kiswahili sanifu na hatimae msamiati wa asili wa lahaja ya Kimakunduchi umeachwa kabisa kimatumizi au kutumika sambamba na ule ulolioibuka.

Kutokana na mwiningilio wa Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi, kuna msamiati ambao hautumiki ipasavyo katika jamii hiyo. Athari hii ya kutotumia baadhi ya msamiati mara kwa mara kama ilivyokuwa kawaida ya

matumizi yake, imesababishwa na mambo mengi bali la msingi zaidi ni mwingilio wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti ulionesha kuwa katika nyanja zote za kimaisha Kiswahili sanifu kinatumiwa na kudhoofisha matumizi ya Kimakunduchi. Kwa hivyo, kuna msamiati umeibuka na kutumika na vijana na kuna msamiati ambao hautumiki kikawaida kama ulivyokuwa ukitumiwa na wazee hapo kabla. Mabadiliko hayo yamegusa katika nyanja zote za kimaisha zikiwemo: za utamaduni, biashara, elimu, kijamii na hata kisiasa; kama inavyochambuliwa hapo chini:

#### **4.3.1 Msamiati Ulivoachwa na Ulivoibuka Katika Uwanja wa Elimu**

Utafiti ulibaini kuwa, uwanja wa elimu ndio ambao unaongoza katika kutilia mkazo matumizi ya Kiswahili sanifu. Walimu na wanafunzi hulazimika kutumia Kiswahili sanifu kwa sababu ndio lugha rasmi inayokubalika kutumika katika uwanja wa elimu. Data zilionesha kuwa kutumia lahaja ya Kimakunduchi ambayo si rahisi kueleweka kwa wasiokuwa Wamakunduchi ni kupoteza lengo la elimu. Kwa hivyo, utambuzi wa Kiswahili sanifu ndio jambo la msingi litakalowawezesha wanafunzi kufaulu masomo yao.

Hojaji zilizogawiwa kwa wasomi ambaoni wanafunzi zilionesha kuwa wanafunzi walishindwa kuyajua maneno yaliyotakiwa kwa lahaja ya Kimakunduchi. Maneno hayo yaliandikwa kwa Kiswahili sanifu na kuwataka wanafunzi wayaandike kwa Kimakunduchi. Maneno hayo ni; mwanafunzi, kufaulu, kufeli, mwalimu, mtahani na mengine kama hayo.

Matokeo yalionesha kuwa kati ya wasomi ishirini na tano waliojibu, ni wasomi tisa ndio ambao walijaribu kujibu baadhi ya maneno hayo na kumi na nne waliobaki walishindwa kuyajibu maneno hayo. Kwa tafsiri hiyo, ni wazi kuwa kuna maneno ambayo yameibuka na mengine yameachwa kutoka katika lahaja ya Kimakunduchi na hayatumiki kama yalivyokuwa kabla.

Mbinu ya pili iliyotumika ni mahojiano, katika mbinu hii, mtafiti alitumia sentensi kwa kuyatumia maneno hayohayo. Sentensi zilikuwa katika lahaja ya Kimakunduchi na kuwataka wasailiya kuzibadilisha na kuwa katika Kiswahili sanifu. Sentensi zilizotumiwa ni kama ifuatavyo:

- i) Viyatuyake vyaga
- ii) Kiya akakwa huyagisa
- iii) Ugonjwa umtuu kitako.

Katika mbinu hii utafiti ulibaini kuwa wanafunzi na vijana wengine walioulizwa walikuwa wakisitasita kutolea maana. Wengi mionganini mwao walishindwa kuwa na maana ya uhakika. Kwa hivyo, ni kusema kuwa baadhi ya msamiati huo ulionekana ni mgumu kwa wanafunzi walioshiriki na kutoa tafsiri kuwa kuna msamiati wa Kimakunduchi ambao umeibuka na ambao umepotea kwa kutotumiwa na wanajamii hao. Tafsiri za maneno na sentensi hizo ni kama ifuatavyo:

- i) Viyatuyake Vimepotea
- ii) Kila akipewa Hupoteza
- iii) Ugonjwa wa mtu kitako

Kutokana na mfumo wa elimu rasmi kuwa ni mfumo mpya ndani ya jamii ya Makunduchi, utafiti ulibaini kuwa misamiati iliyoibuka kutokana na mfumo huu ni mingi kuliko ile iliyoachwa katika nyanja hii. Hivyo jadweli la hapo chini linaonesha msamiati ulioibuka katika nyanja ya kielimu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi, kama jedwali na 4.1 linavyoonesha hapa chini.

#### **Jedwali 4.1: Msamiati Ulolioibuka Katika Uwanja wa Elimu**

<b>Na.</b>	<b>Neno lililoibuka</b>	<b>Neno lililoachwa</b>
1	Kuanguka	Kugwa
2	Kufeli	—
3	Kufaulu	—
4	Hodari	—
5	Mtoro	—
6	Mjadala	—
7	Kufoji	—
8	Wanafunzi	—
9	Walimu	—
10	Vitabu	—
11	Kusaidia	—
12	Kilaza	Bite

Matokeo katika jadweli hili yanaonesha kuwa kuna msamiati mwangi ambao umeibuka na kutumika katika lahaja ya Kimakunduchi hasa katika nyanja hii ya elimu, kuliko hata ile iliyoachwa. Hali hii inatokana na ukweli kuwa mfumo wa kutolea elimu uliotumika na jamii ya Makunduchi kabla ya mfumo huu ni tofauti kabisa na mfumo huu wa elimu ya mkondo rasmi. Utafiti ulibaini kuwa jamii ya watu Wamakunduchi walitumia mazingira ya uvuvi zaidi katika kuwafundisha wavulana wao na kutumia mazingira ya shamba katika kuwafundisha wasichana wao. Hivyo walitumia zaidi maneno kama *sarahangi* kama ni mvulana

anayefundishwa, matwesi na uvuvi na *muwizi* kama msichana anayefundishwa kuwinga wanyama wasile mazao ya ukulima. Maeneo mengine ya kujifunza ilikuwa ni singo, hiki kilikuwa ni chuo cha masuali ya ndoa. Maneno mengine yaliyotumika katika elimu kabla ya elimu ya mkondo rasmi ni kama fundi, ngariba, na nahoza . Elimu hii imetolewa kwa vitendo zaidi kuliko nadharia.

#### **4.3.2 Msamiati Ulloibuka na Ulloachwa Katika Uwanja wa Utamaduni**

Utamaduni ni kipengele muhimu ambacho huigusa jamii kwa upana zaidi. Kipengele hiki hujihusisha na mambo mengi yanayohusu jamii katika nyanja zote za maisha. Katika kipengele hiki, utafiti ulijikita katika kuangalia lugha ilivyotumika na athari za mabadiliko yake. Utafiti umebaini kuwa kuna msamiati wa kiutamaduni ambao ulikuwa ukitumika katika shughuli zilizohusu mambo ya kiutamaduni ambao umeachwa kutokana na kuingiliwa na Kiswahili sanifu. Uachaji huo umetokana ama na shughuli hizo kutawaliwa na uhamiaji wa watu, sherehe hizo kufanywa ni za kitaifa au athari iliyotokana na matumizi ya msamiati kielimu.

Msamiati ulioachwa katika lahaja ya Kimakunduchi katika kipengele cha utamaduni umejitokeza katika nyanja tofauti za kiutamaduni kama ifuatavyo:

##### **4.3.2.1 Msamiati Ulloibuka na Ulloachwa Katika Michezo ya Watoto**

Watoto ni sehemu muhimu ya jamii inayopokea mabadiliko ya jambo kwa haraka zaidi. Mabadiliko yanayojiteza kwa watoto yana athari kubwa kutokana na mazowea yanayojengeka kwa haraka na kuchelewa kuondoka. Utafiti umebaini kuwa katika michezo ya watoto kuna msamiati wa Kimakunduchi ulikuwa umezoleka ambao umeachwa, pia upo msamiati ambao umeibuka kuititia nyanja hii

ya michezo ya watoto. Michezo hii imeathirika kutokana na uhamaji na uhumiaji wa watoto na kuchanganyika na jamii nyingine hususan ile inayotumia Kiswahili sanifu. Pia, kuibuka na kuachwa kwa kusababishwa pia na mfumo wa kielimu ambao unawataka watoto kutumia Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa nyimbo zilizoimbwa na michezo iliyochewa ilitumia Kiswahili sanifu zaidi kuliko lahaja ya Kimakunduchi. Miiongoni mwa msamiati ulioachwa katika uga wa michezo ya watoto ni kama vile; “uwa msomusomu,” “wisha,” “kavwaa,” “ikavita” na “hamba.” Maneno hayo yalibainika kutotumika kama yalivyokuwa yaktumika kabla. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa, watoto wanatumia maneno ya Kiswahili sanifu ambayo yamechukuwa nafasi ya maneno hayo yaliyotajwa. Maneno hayo yanatumika kama ifuatavyo:

“Uwa msomusomu” neno lenye maana ya kuwa ni msafi katika Kiswahili sanifu na kwa sasa neno “uko msafi” ndilo ambalo linatumika zaidi badala ya uwa msomusomu. “wisha” lina maana ya ‘ondosha katika mchezo ambao mtoto mmoja hutakiwa aondoshe mkono wake kwa kuambiwa hivyo. Katika utafiti, neno ondosha ndilo ambalo lilisikika kutumika badala ya neno ‘wisha’ ambalo ndio neno la asili katika mchezo huo. “Ikavita” lina maana ya ‘ikipita’. Neno hilo lilipatikana katika mchezo wa meli, ambapo badala ya neno hilo lililotumika kiasili katika mchezo huo, sasa neno ‘ikipita’ ambalo ni la Kiswahili sanifu ndilo ambalo hutumika katika mchezo huo. Pia neno “Hamba” halitumiki na neno “kama” la Kiswahili sanifu ndilo linalotumika kwa sasa na “Kugwa” lenye maana ya maana ya kuanguka, katika uchunguzi uliofanyika, watoto walitumia neno ‘kuanguka’ badala ya kugwa. Manneno mengine ni kama yalivyoanishwa kwenye jdwali na. 4.2 hapa chini.

**Jedwali 4.2: Maneno ya Kiswahili Sanifu Yanayotumika Katika Nyimbo za Michezo ya Watoto za Lahaja ya Kimakunduchi**

<b>Na.</b>	<b>Msamiati mpya ulioibuka</b>	<b>Msamiati wa Kimajunduchi ulioachwa wa Kiswahili sanifu</b>	<b>Mchezo Husika</b>
1	Uko safi	Uwa msomusomu	Mchicha
2	Tutaishi	Tuchaishi	Kitambaa cheupe
3	Haipo	Haivo	Kifanifani
4	Ondosha	Wisha	Kifanifani
5	Nipe	Nka	Kibibi nipe maji
6	Nitakupa	nchakuka	kibibi nipe maji
7	na wewe unalo	nawe kunalyo	kifichoficho
8	Kavaa	Kavwaa	Mwanajumbe
9	Ikipita juu	Ikavita juu!	Meli
10	Hapa hayupo, hapa hayupo!	Vano havo, vano havo!	Saka mke wangu
11	Kampa	Kamka	Saka mke wangu
12	Kama	Hamba	Mume kasafiri
13	Hapa pana nini?	Vano vana nini?	Meli
14	Mtukufu wa kiume	Danga dume	Kitikiti

Tafsiri ya matokeo hayo ni kwamba, kipengele cha utamaduni kwa watoto kimekuwa na muathiriko wa Kiswahili sanifu ambao umesababisha kuachwa kwa baadhi ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi. Athari hiyo imetokana na mwingilio wa Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi.

#### **4.3.2.2 Msamiati Ulloibuka na Ulloachwa Katika Shughuli za Harusi**

Shughuli za harusi hujumuisha watu wengi wenye matumizi tofauti ya lahaja. Kama ilivyobainishwa katika 4.2.5 kuwa kuna sababu ya uhamiaji ambayo husababisha kuwa na matumizi yaliyotofauti na lahaja ya Kimakunduchi. Kwa hivyo, utafiti ulibaini kuwa kuna msamiati ulloachwa katika nyimbo zilizotumika katika sherehe za harusi na kubainika kuwa ultumika msamiati wa Kiswahili sanifu badala ya Kimakunduchi kama jedali na. 4.3 hapa chini linavyoonesha.:

### **Jedwali 4.3: Msamiati Uliaoachwa Katika Sherehe za Harusi**

<b>Na.</b>	<b>Neno la Kimakunduchi lilioachwa au kutumika sambamba na maneno yaliyoibuka</b>	<b>Maneno yaliyoibuka kutokana na Kiswahili sanifu</b>
1	Lyungo	Ungo
2	Kuvyaa	Kuzaa
3	Siyagomo	Siyataki
4	Kwacha kosa	Kuacha kuosha
5	Njo	Ndio
6	Ukachaka	Ukitaka
7	Dumba	Kubali
8	Twaa	Kujamiihana
9	Wehu	Mcharuko
10	Chozi	Cheche
11	Utondo	Raha

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mwingilio wa Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi umejiingiza katika sekta zote za kimaisha na kuathiri. Sherehe za harusi zina athari kubwa kwa jamii kwani nyimbo za harusi huwavutia watu wengi kuzisikiliza na kuziiga. Kipengele hiki cha sherehe hujumuisha watu wengi na uwenezi wa lugha inayotumika unakuwa mkubwa. Kwa hivyo, athari ya Kiswahili sanifu inajitokeza kwa upana zaidi kupitia sherehe za harusi.

#### **4.3.3 Msamiati Uliaoibuka na Uliaoachwa Katika Makundi ya Kijamii**

Katika jamii na mambo yake ya kila siku kumekuwa na muathiriko wa lahaja ya Kimakunduchi ulisababishwa na mwingilio wa Kiswahili sanifu. Athari hiyo ambayo imeikumba jamii kijumla imesababisha msamiati wa Kimakunduchi kuachwa kabisa au kutokuwa na matumizi kama ilivyokuwa kabla. Katika sehemu hii, imebainika kuwa kuna msamiati wa Kimakunduchi ambao umeachwa. Msamiati huo umegawiwa kwa mujibu wa data zilivyokusanywa:

#### **4.3.3.1 Msamiati Ulloibuka na Ulloachwa kwa Upande wa Akina Mama**

Kwa upande wa akina mama kuna msamiati wa Kimakunduchi ambao haukutumiwa na watafitiwa. Msamiati huo ulikuwa na mbadala kutoka katika lahaja ya Kiswahili sanifu. Msamiati ulichunguzwa ni kama vile; kifuu, kumwaga, chochea, kujitapisha, kupoteza, na kusaidia. Maneno hayo yalioneckana kuwa ni mageni hasa kwa watafitiwa walio kati ya umri wa miaka kumi na tisa hadi thelathini na mbili. Watafitiwa walibabaika katika kuyatolea maana na kati ya watafitiwa ishirini na tatu, ni watafitiwa saba tu ndio ambao waliweza kutoa baadhi ya msamiati huo kwa lahaja ya Kimakunduchi.

#### **Jedwali 4.4: Msamiati Ulloachwa Katika Miiongoni mwa akina Mama**

Na.	Msamiati ulloachwa	Msamiati Ulloibuka
1	Kipangaa	Kifuu
2	Kumalwa	Kumwaga
3	Kokanya	Chochea
4	Gauwa	Kujitapisha
5	Kwagisa	Kupoteza
6	Kumwavwa	Kusaidia
7	Mfanigo	Uchuro
8	Tapo	Makopa
9	Manyezi	Huruma
10	Ukoga	Mabaki ya kula katika meno
11	Vwende	Papai bivu sana
12	Choa	Vitu vidogo vidogo
13	Too	Sana
14	Koka	Nyonya
15	Ngaa	Mwangaza
16	Wanakele	Watoto
17	Sheshenduka	Kujishauwa
18	Kwenje/kooma	Koroma
19	Koromanya/kolomanya	Mseto
20	Popotoa	Vunja
21	Fyufyuta	Fukuchika

Maneno yaliyotumika kama kifuu, kumwaga, chochea, kujitapisha, kupoteza, na kusaidia ni maneno ya Kiswahili sanifu ambayo yameibuka na kutumika badala ya

maneno; kipangaa, kumalwa, kokanya, gauwa, kugisa, na kumwawwa. Maneno yaliyoachwa na yale yaliyotumika badala yake ni kama yanavyooneshwa katika jedwali na. 4.4 hapo juu.

Jadweli 4.4 linadhihirisha kuwa kumekuwa na uachaji wa msamiati wa Kimakunduchi kutokana na mwingilio wa Kiswahili sanifu. Msamiati wa asili umekuwa ukiachwa na kubadilika kutokana na msamiati ambao unaingizwa katika lahaja hiyo kutoka katika Kiswahili sanifu

#### **4.3.3.2 Msamiati Ulioibuka na Ulioachwa kwa Upande wa Vijana wa Kiume**

Kwa mujibu wa Ali (2016), vijana ndio kundi ambalo huchukua mabadiliko kwa haraka zaidi. Mtafiti huyo amebainisha kuwa kundi la vijana ndilo ambalo hukimbilia kutumia Kiswahili sanifu na kuacha kutumia lahaja kutokana na mwingiliano wao kimawasiliano na watu wa sehemu mbalimbali. Alieleza kuwa vijana huona haya kuzungumza lahaja yao na kuamua kutumia Kiswahili sanifu ili kuepuka usumbufu wowote ule ambao wanadhani kuwa unaweza kuwapata.

Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa vijana wanakuwa na mabadiliko ya utumiaji wa lahaja na kugeukia katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, mtafiti aliwatumia vijana ili kupata data zitakazoogoza kuona uwachwaji wa msamiati wa Kimakunduchi mionganini mwa vijana. Mtafiti alitumia maneno; tazama/ona, topeni, njaa (kali), kazana na nagasia. Utafiti ulibaini kuwa vijana watano kati ya vijana kumi na saba ndio ambao waliweza kutoa msamiati halisi wa baadhi ya maneno

hayo, na vijana kumi na mbili walishindwa kutoa msamiati halisi wa Kimakunduchi kwa maneno yaliyotolewa.

#### **Jedwali 4.5: Msamiati Uliaoachwa Miongoni mwa vijana**

Na.	Msamiati uliachwa	Msamiati ulioibuka
1	Lola	Tazama/ona
2	Tovsky	Topeni
3	Chagaa	Kazana
4	Ujoma	Njaa (kali)
5	vivumbwe	Vichaka
6	Ngasia	Kimilia
7	Tota	Kuzama baharini
8	Chama	Kinyesi
9	Zezeta	Pesa ya shaba
10	Chavua	Mataka ya baharini
11	Chwapu	Fimbo ya kupigia mtoto
12	Izaiza	Sitasita
13	Mwenye hofu	Majechejeche
14	Uka	Ondoka
15	Ng'wang'uka	Hamakia
16	Kukwa	Kupewa
17	Vyuvyuza	Chelewesha
18	Mbilinganya	Mbabaishaji
19	Temka	Pwelewa
20	pwecheka	Kujiachia
21	mbombambomba	maiti hai
22	Kuvukutwa	Maumivu (ya ndani)
23	Kukefya	kupepesa

Vikao vya baraza za karata na mazungumzo vilitawaliwa na vijana wengi. Vikao hivyo vilikuwa na utofauti wa mazungumzo na wazungumzaji. Katika kuchunguza matumizi ya msamiati wa Kiswahili sanifu kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi, ilibainika kuwa wazungumzaji wengi walitumia Kiswahili sanifu kuliko lahaja ya Kimakunduchi. Kwa mfano, mtafiti alitumia wasaidizi katika vikao vya bao na karata ili kupata maelezo yaliyokuwa yakizungumzwa. Kwa mujibu wa

kinasa sauti kilichotumika katika vikao hivyo, vijana walio wengi walitumia Kiswahili sanifu mara nyingi zaidi kuliko Kimakunduchi. Matokeo haya ni kubainisha kuwa kuna maneno mengi ya Kimakunduchi ambayo kwa hivi sasa hayajulikani au hayatumiki sana katika mazungumzo ya kila siku ya Wamakunduchi. Msamiati halisi wa maneno hayo ni kama unavyooneshwa katika jedwali 4.5 hapo juu.

Tafsiri ya matokeo hayo ni kwamba, vijana ambao ndio wanaotegemewa kuikuza na kuiendeleza lahaja ya Kimakunduchi wamekuwa ndio waathirika wakubwa wa mwingilio wa Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, lahaja hiyo inapoteza msamiati wake siku hadi siku na kutawaliwa na Kiswahili sanifu.

#### **4.3.4 Msamiati Ulloibuka na Ulloachwa Katika Uga wa Habari**

Tasnia ya habari ina mawanda makubwa katika kukuza au kudhoofisha lugha. Kupitia tasnia hiyo, lugha huweza kujitangaza na kuwa na mawanda ya watumiaji. Kwa hivyo, kukua na kuenea Kiswahili sanifu kumesababisha lahaja ya Kimakunduchi kuacha kutumia msamiati ambao unaakisi uga wa mawasiliano katika uwanja wa habari. Kuna maneno kama vile; dafya, lenye maana ya shinda/pata ushindi, fyokchoo lenye maana ya kubaka, fyalalika kwa maana ya kukimbia, kweleka, lenye maana ya kubeba na kicheucheu, kwa maana ya kuwa tayari.

Neno ‘dafya’ linatumika katika habari za michezo kuonesha kuwa timu moja imeishinda nyengine katika mpambano wao. Kwa mfano, Nyoka mweusi idafyu goli moja. Neno ‘fyokchoo’ hutumika zaidi katika habari za kijamii kuonesha tendo la

kubaka. Neno fyalalika linatumika katika habari za michezo na habari za kijamii pia. Neno hilo lina maana ya kimbia. ‘Kweleka’ hutumika katika habari za kijamii kwa maana ya kubeba. Na neno kicheucheu hutumika katika habari za kijamii kwa maana ya kuwa tayari.

Utafiti umegundua kuwa msamiati wa Kimakunduchi ulioorodheshwa hautumiki mara kwa mara katika tasnia hiyo ya habari kwa sasa. Kwa hivyo, maneno dafya, fyalalika, kicheucheu, fyokochoo na kweleka hayatumiki badala yake hutumika maneno, shinda/pata ushindi, kubaka, kukimbia, na kubebe. Maneno ambayo yanatumika kwa sasa ni kutoka katika Kiswahili sanifu.

#### **4.4 Athari za Kiswahili Sanifu Katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi**

Katika lengo hili la tatu utafiti uliazimia kutathmini athari iliyopo kutokana na mwingilio wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi. Matokeo ya tathmini yalipatikana kutokana na data zilizokusanywa kutoka katika makundi ya watafitiwa na data za maktabani. Mtafiti alitilia maanani data zote zilizotolewa kwa kuchambuwa kwa undani makusudio ya kila data ili kubaini mustakbali wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na mwingilio wa Kiswahili sanifu unavyoendelea kushika kasi na kutumika katika shughuli zote za kimaisha kwa jamii ya Wamakunduchi.

Mchanganuo wa athari ya Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi pia ulizingatia nafasi ya Kiswahili sanifu katika uwanja wa mawasiliano duniani. Kiswahili sanifu imekuwa ni lugha inayotumika katika mikutano ya Umoja wa Afrika, inatumika katika vyomo mbalimbali vya habari duniani, inatumika katika kutolea elimu, inasomeshewa wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili, inatumika

katika shughuli za serikali na ina mawanda makubwa ya watumiaji. Kutokana na hali hiyo, Kiswahili sanifu kimekuwa na nafasi kubwa kimawasiliano na upana wa matumizi na watumiaji.

Kutokana na maelezo hayo yaliyotangulia, ni wazi kuwa mwilingio wa Kiswahili sanifu uliojitokeza katika lahaja ya Kimakunduchi, unaathiri ukuaji wa lahaja hiyo. Kwa hivyo, lengo hili limejikita katika kuonesha athari zilizobainika katika utafiti huu kama ifuatavyo:

#### **4.4.1 Kupotea kwa Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi**

Utafiti umebaini kuwa mwilingio wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi, umesababisha kupotea msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi. Hii ni kama ilivyobainika kuwa msamiati wa Kimakunduchi hautumiki kama ambavyo ulikuwa ukitumika kabla. Utafiti umebaini kuwa mabadiliko ya kimsamiati kutoka ule wa Kimakunduchi na kuwa wa Kiswahili sanifu umejitokeza katika nyanja zote za kimaisha. Matokeo hayo yameathiri lahaja ya Kimakundi kuitia makundi mbalimbali kama ifuatavyo:

##### **4.4.1.1 Athari Iliyojitokeza Katika Uwnja wa Elimu**

Katika uwanja wa elimu ndiko ambako athari ya Kiswahili kwa lahaja ya Kimakunduchi ilikobainika zaidi. Katika sehemu hii, wanafunzi hulazimika kutumia Kiswahili sanifu ili kulingana na wengine kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Utafiti umebaini kuwa juhudhi kubwa hufanyika tokea katika shule za chekechea hadi sekondari kuhakikisha kuwa watoto wanatumia Kiswahili sanifu na sio lahaja ya

Kimakunduchi. Athari iliyobainika ni kuwa, watoto huathiriwa na matumizi ya Kiswahili sanifu na kuacha taratibu msamiati wa Kimakunduchi. Jambo hilo nilazima kufanyika kwani wanafunzi wanatakiwa kujibu mitihani yao kwa kutumia Kiswahili sanifu na sio Kimakunduchi ambacho kinaeleweka na wenyewe Wamakunduchi pekee.

Tafisiri ya matokeo hayo ni kuwa wanafunzi na walimu ambao wanakitumia Kiswahili sanifu huathirika na kuwa watumiaji wa Kiswahili sanifu badala ya Kimakunduchi.

#### **4.4.1.2 Athari Iliyojiteza Katika Michezo ya Watoto**

Kwa upande mwengine, matumizi ya Kiswahili sanifu katika michezo ya watoto ambayo ndio chanzo muhimu cha ukuzaji wa lugha, kumeathiri sana lahaja hiyo. Nukata hii inatokana na imani kuwa watoto huibukia kile walichofahamia. Kwa hivyo, watoto ambao wamekuzwa na misingi ya kutumia lugha sanifu ya Kiswahili, hawatarajiji kuwa ni watumizi wazuri wa lahaja ya Kimakunduchi.

Watoto ni sehemu muhimu ya ukuzaji wa lugha katika jamii. Kwa hivyo, wanapokosa msamiati wa lahaja yao tokea mapema, ni vigumu kuwapatia na kuwawezesha kuitumia vizuri lahaja hiyo wakati wamekuwa wakubwa. Michezo ya watoto kama ilivyobainishwa katika lengo la pili (4.3.2.1), kuwa kuna msamiati wa Kimakunduchi ambao umeachwa na badala yake msamiati wa Kiswahili sanifu ndio unaotumika. Msamiati usitumika kwa sasa ni kama vile; “uwa msomusomu,”

“wisha,” “kavwaa,” “ikavita” na “hamba.” Na badala yake msamiati wa Kiswahili sanifu kama; uko safi, ondosha, kavaa, ikipita na kama, ndio yanayotumika.

Matokeo hayo ni kama yalivyoelezwa katika msingi wa kwanza wa nadharia iliyotumika katika utafiti huu kuwa, Lugha au lahaja zenyenye uwiano na ukaribu wa kilugha zina uwezekano mbubwa wa kuathiriana kimsamiati, maana, lafudhi na mjengeko wa muundo wa lugha kijumla. Matokeo hayo hujitokeza zaidi kwa lugha au lahaja inayoathiriwa kupoteza msamiati wake na kuchukuwa msamiati wa lahaja iliyooizidi nguvu na mawanda ya utumizi. Hivyo, ni wazi kuwa lahaja ya Kimakunduchi inaendelea kupoteza msamiati pale ambapo Kiswahili sanifu kinazidi kutanua mawanda ya matumizi yake.

#### **4.4.1.3 Athari Iliyojitekeza Katika Maongezi ya vijana**

Utafiti uligundua kuwa vijana ndio kundi ambalo limeathirika zaidi na matumizi ya Kiswahili sanifu. Suala hilo husababishwa hasa mwingiliano wa vijana wa sehemu moja na vijana wa sehemu mbalimbali. Mberwa (keshatajwa) ameeleza kuwa vijana ni watu wa kuchanganyika na watu mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Kutokana na mwingiliano huo, vijana walio wengi huona tabu kutumia lahaja zao mbele ya watu ambao si wenyeji wa sehemu walizotoka. Akitolea mifano anasema kuwa, kwa mfano vijana wa Tumbatu waliopitia katika vyanzo vya elimu na kukutana na wenzao wanaotoka sehemu za mji wa Unguja, hujisikia aibu kuzungumza Kitumbatu. Inawezekana ni kujiona ‘washamba’ au si Waswahili safi. Kutokana na maelezo hayo, athari ya Kiswahili sanifu huonekana kuhatarisha lahaja za Kiswahili, kwa vile kiungo muhimu cha wakuzaji wa lahaja hiyo kutokuwa tayari

kuitumia popote wanapokuwa. Matokeo hayo ni kama yalivyobainishwa katika msingi wa pili wa nadharia iliyotumika katika utafiti huu kuwa, Mwingiliano wa lugha au lahaja unaweza kuidhoofisha au kuiua lahaja moja. Lahaja inayoathirika kwa kiasi kikubwa inakuwa hatarini kupoteza uhalisia na kusababisha kudhoofika na pengine kufa.

#### **4.4.1.4 Athari Iliyojitokeza Katika Shughuli za Kiutamaduni**

Utamaduni ni sehemu muhimu ya utambulisho wa jamii. Kipengele hiki cha utamaduni hujumuisha mambo yote ya kimaisha katika jamii, ikiwemo lugha. Hivyo basi, matumizi ya lugha husaidia kumjua mtu ni kutoka wapi kama ambavyo hujibainisha kwa mambo mengine ya kitamaduni. Kutokana na mwingilio wa Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi, alama ya utamaduni wa Kimakunduchi imekuwa na udhaifu. Hii ni kwa sababu katika shughuli za kiutamaduni kama vile katika sherehe za ‘Mwaka Kogwa’ Kiswahili sanifu huchukuwa nafasi muhimu ya mawasiliano.

Urasmi wa sherehe za mwaka kogwa, umezifanya sherehe hizo kutekwa na Kiswahili sanifu tokea katika utambulisho hadi katika kuendelea na sherehe zenyewe. Lengo la yote hayo ni kuwawezesha wageni waalikwa kufahamu yote yanayosemwa katika shughuli hiyo. Hatima ya hayo ni kupotea msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika kila kipengele cha maisha.

#### **4.4.2 Kupoteza Vyanzo vya Msamiati wa Kiswahili Sanifu**

Lahaja za Kiswahili ni vyanzo muhimu katika ukuaji wa Kiswahili sanifu. Uwepo wa lahaja hizo, huchangia kuongeza msamiati ambao una asili ya Waswahili wenyewe.

Panapokuwa na mahitaji ya msamiati mpya kutokana na jambo jipya lililoingia au utata wa matumizi kwa msamiati uliopo, lahaja huweza kutumika kwa lengo la kusaidia kupata neno ambalo litafaa kwa sehemu husika.

Maganga (keshatajwa) anasisitiza kuwa usanifishaji haukuwa na maana kuwa huo ulikuwa ndio mwisho wa lahaja nyingine za Kiswahili, hasha, lahaja ziliendelea na kuwa ni chanzo muhimu cha kukuza msamiati wa Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa kauli hiyo, ni wazi kuwa lahaja zina nafasi muhimu katika ukuaji wa Kiswahili sanifu. Mchango wa lahaja ndio ambao unakifanya Kiswahili sanifu kukua, kujitegemea na kuwa na msamiati utakaotosheleza katika mahitaji ya mawasiliano katika nyanja zote za kimaisha. Lahaja za Kiswahili zinapokuwa na udhaifu wa msamiati, huinyima lugha hiyo nafasi ya kujitanua na kukua kwa kupata msamiati ambao unaweza kuziba pengo na kuiimarisha lugha.

#### **4.5 Muhtasari wa Sura**

Sura hii imewasilisha mjadala wa matokeo na uchanganuzi wake. Kwenye sura hii, kuna uwasilishwaji wa matokeo ya utafiti kama yalivyokusanywa kutoka uwandani na maktabani. Matokeo yamejumuisha data ambazo zilikusanywa kutoka kwa wazawa na wakaazi wa Makunduchi pamoja na wataalamu wa lahaja ya Kimakunduchi.

Sura hii imeweka bayana mabadiliko ya msamiati wa Kimakunduchi ambao kwa kiasi kikubwa umechangiwa na mwingilio wa Kiswahili sanifu kwa lahaja ya Kimakunduchi. Data zilizokusanywa zilibainisha kuwa kuna mabadiliko ya msamiati

katika lahaja ya Kimakunduchi. Mabadiliko hayo yametokana na kuibuka kwa msamiati wa Kiswahili sanifu unaotumika katika lahaja ya Kimakunduchi. Aidha, utafiti ulichunguza na kubaini kuwa kuna msamiati wa kale wa Kimakunduchi ambao kwa sasa hautumiki kama ulivyokuwa ukitumika hapo kale. Hii ina maana kuwa kuna msamiati ulioachwa, mwisho ni kuwa utafiti ulijikita kutathmini athari za mwingilio wa Kiswahili sanifu kwa msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi.

## SURA YA TANO

### **5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Muhtasari**

##### **5.1.1 Muhtasari wa Jumla**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuuchunguza Athari ya Kiswahili Sanifu Katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti ulichunguza ni kwa kiasi gani mwilingilio wa Kiswahili sanifu ulivyoweza kuwa na athari kwa lahaja ya Kimakunduchi. Utafiti ulikuwa na lengo la kuchunguza uwezekano wa uhai au upotevu wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maendeleo ya ukuaji wa Kiswahili sanifu ulivyoshika kasi na kutumika duniani katika nyanja mbalimbali. Kwa hivyo, utafiti ulidhamiria kufikia lengo kuu la utafiti kwa muongozo wa malengo mahsusini ya utafiti ambayo ni:

Kwanza, Kubainisha njia zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu. Pili, Kubainisha msamiati ulioachwa kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi. Na tatu, ni Kutathmini athari za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi.

Katika kukusanya data za na kupata matokeo, utafiti ultimia maswali yaliyoendana na malengo mahsusini ambayo ni; kwanza, Ni msamiati gani ulioibuka kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya kimakuinduchi? Pili, Kuna msamiati upi ulioachwa kutokona na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya

Kimakunduchi? Na tatu, Kuna athari gani za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi?

Kutokana na azma ya kufikia lengo la utafiti na kupata matokeo yatakayothibitisha dhana iliyolengwa katika utafiti huu, nadharia ya Muathiriano wa Lugha ilitumika. Mtafiti aliteua nadharia hiyo kwani aliona ni faafu katika kubaini mabadiliko ya mawasiliano na mitindo ya matumizi ya misamiati katika lugha husika. Nadharia hiyo pia imesaidia kubaini msamiati ulioibuka na ulioachwa katika lahaja ya Kimakunduchi. Nadharia hiyo iliwezesha kufanikisha uchambuzi wa data zilizokusanywa na kufikia malengo ya utafiti.

Data hizi zilikusanywa kwa njia mbali mbali mbali zikiwemo, mahojiano, mjadala wa vikundi, ushuhudiaji na hojaji. Utafiti huu ulifanyika uwandani kwa kuitia sampuli ya wazee, vijana na wasomi. Sampuli hii ilipatikana kwa njia ya usampulishaji wa unasibu na wa kundi lengwa. Pia, ulifanyika maktabani kwa kuitia marejeo mbali mbali yanayohusiana na mada hii. Data zilizopatikana katika utafiti huu zilichambuliwa kwa mkabala wa kiufafanuzi. Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Makunduchi kwa kugawiwa kanda tatu kuu; kanda ya Makunduchi, kanda ya juu na kanda ya pwani. Kanda zote hizi zimeweza kujengwa na shehia tofauti. Njia na mbinu hizi za ukusanyaji wa data zimesaidia sana kufikia malengo ya utafiti huu na kufikia matukio yaliyochambuliwa katika tasnifu hii.

### **5.1.2 Muhtasari Wa Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti yalipatikana kutokana na data zilizokusanywa kutoka kwa wazawa, wakaazi na wataalamu wanaoifahamu lahaja ya Kimakunduchi. Matokeo

hayo yalisaidia kujibu masuali ya utafti ambayo ndiyo yalikuwa dira ya utafiti wenyewe. Masuali yaliyoongoza utafiti na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

Swali la kwanza la utafiti lilikuwa: Ni njia gani zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano ya Kiswahili sanifu? Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa kuna njia mbalimbali zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maingiliano wa Kiswahili sanifu, miongoni mwa njia hizo ni:- njia ya mwingiliano kupitia vyombo vyaa habari, mwingiliano kupitia elimu, mwingiliano kupitia utamaduni, mwingiliano kupitia biashara, mwingiliano kupitia uhamiaji na uhamaji, muingiliano kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vyaa mawasiliano. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa njia hizo ndizo zilizotumika kuathiri msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi kupitia maingiliano ya Kiswahili sanifu.

Swali la pili lilikuwa: Kuna msamiati upi ulioachwa kutokona na maingiliano ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi? Matokeo yaliyopatikana katika suali hili yalibainisha kuwa kuna msamiati ambao ulikuwa ukitumika kabla na ulikuwa ni maarufu sana kwa wazee ambao kwa sasa umekuwa hautumiki kama ulivyokuwa ukitumika kabla. Kwa hivyo, matokeo yamebainisha kuwa kumekuwa na tofauti kubwa ya matumizi ya msamiati wa Kimakunduchi kwa sasa. Watu wengi na hasa vijana waliopata elimu hawatumii msamiati wa Kimakunduchi katika mazungumzo yao. Athari hii imetokana na mfumo wa elimu ambao umewajenga watoto wanaosoma shule kutumia Kiswahili sanifu katika masomo yao.

Suali la tatu lilikuwa: Kuna athari gani za Kiswahili sanifu katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi? Watafitiwa waliojibu suali hili walibainisha kuwa, lahaja za lugha ya Kiswahili kikiwemo Kimakunduchi, zinakabiliwa na wakati mgumu katika kudumu kwake. Watafitiwa wengi waliamini kuwa Kimakunduchi pamoja na lahaja nyengine zinakabiliwa na hatari ya kupotea kutokana na wimbi kubwa la uenezi wa Kiswahili sanifu na utanuzi wa mawanda yake ya kimatumizi duniani kote. Kutokana na kuenea kwa Kiswahili sanifu katika vyombo vyahabari, katika masuala ya kielimu na mitandao ya kijamii. Watafitiwa walioshiriki walionesha wasiwasi wa kuwepo kwa lahaja ya Kimakunduchi kadri muda unavyoendelea.

## **5.2 Hitimisho**

Utafiti huu umethibitisha wazi kuwa upo muingiliano mkubwa wa Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi. Hali hii inatokana na masuali mbali mbali yakiwemo ya kimaendeleo ya kijamii pamoja na mawasiliano na shughuli za kiuchumi. Utafiti wa huu umesaidia kujua na njia za muingiliano na athari za muingiliano huo, ambazo zimechambuliwa kwa kina katika matokeo ya utafiti huu.

Kwa upande wa matokeo ya utafiti, Mtafiti amebaini kuwa Kimakunduchi kimekuwa na mabadiliko ya msamiati. Kuna msamiati ulioibuka na kutumika sambamba na ule uliokuwepo kabla kwa maana ileile. Pamoja na hilo, kumebainika pia kuwa kuna msamiati ulioachwa katika lahaja ya Kimakunduchi. Msamiati ulioachwa umetokana na sababu nyingi kama vile, uwepo wa matumizi ya lugha rasmi (Kiswahili sanifu) katika masuala ya kielimu, maingiliano ya watu katika masuala ya kibiashara, mawasiliano, habari na uhamiaji wa watu kutoka sehemu moja hadi nyengine.

Hatimaye, utafiti uligundua kuwa kuna hatari ya kudumaa au kupotea kabisa kwa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na kutandawaa na kuenea Kiswahili sanifu katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Maoni ya watafitiwa wengi yalionesha kuwa matumizi ya zana za kisasa kama vile simu, intaneti, mitandao ya kijamii, shughuli za kitaaluma pamoja na vyombo vya habari zinachukuwa nafasi kubwa katika kudumaza na kusababisha kupotea kwa lahaja ya Kimakunduchi.

### **5.3 Mapendekezo**

Baada ya kupata matokeo ya utafiti na uwasilishaji wa uchambuzi uliojitokeza, utafiti huu umekuwa na mapendekezo yaliyojikita katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza, ni mapendekezo ya kukabiliana na changamoto zilizobainika katika utafiti huu na sehemu ya pili, ni mapendekezo kuhusu tafiti zijazo.

#### **5.3.1 Mapendekezo ya Kukabiliana na Changamoto Zilizobainika Katika Utafiti Huu**

Utafiti huu umetoa matokeo yaliyobainisha upungufu wa nguvu za kimatumizi kwa lahaja ya Kimakunduchi na muelekeo wa baadae kwa lahaja hiyo. Matokeo yamebaini mabadiliko ambayo yanatishia kwa kiasi kikubwa uhai wa lahaja ya Kimakunduchi. Hiyo ni athari ya uenezi wa Kiswahili sanifu na mwingilio wake kwa lahaja ya Kimakunduchi. Athari hiyo imejitokeza hasa kwa vijana ambao wameonekana kuwa ndio waathirika wakubwa wa wimbi la matumizi ya Kiswahili sanifu kuliko lahaja ya Kimakunduchi. Msukumo huo uliotokana na uenezi na matumizi ya Kiswahili sanifu, umeiathiri na kuiondolea uasili wake lahaja ya

Kimakunduchi. Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti yalivyojitokeza, utafiti unatoa mapendekezo yafuatayo:

Kuazishwa kwa vyombo vya habari ambavyo vitatoa matangazo yake kwa kutumia lahaja mbalimbali za Kiswahili. Vyombo hivyo ikiwa ni pamoja na redio na televisheni, vitasaidia vijana kuvutika kusikiliza, kuhoji, kuchangia na kutafuta taaluma zaidi kwa kupitia vipindi vitakavyohusiana na lahaja.

- i) Wizara inayohusiana na utamaduni na michezo, ianzishe mijadala, mahojiano na makongamano maalumu ambayo yatakuwa na lengo la kukuza na kuendeleza lahaja za Kiswahili kwa kuwahusisha watu amba ni wamahiri katika kukitamka na kutumia msamiati mwangi wa lahaja husika. Zoezi hili litaleta litaamsha ari kwa watu weledi wa lahaja kuona haja ya kuwasilisha lahaja yao ili ipate kusikika na kufahamika ulimwenguni.
- ii) Wizara ya Elimu ichukuwe juhudzi za makusudi kuhakikisha kuwa wanakamilisha wajibu wao kwa kuzilinda na kuziendeleza lahaja za Kiswahili. Kwa mfano, wizara inaweza kuandaa mashindano ya uwandishi wa hadithi, makala au mashairi kwa kutumia lahaja za Kiswahili. Jambo hili linaweza kushajiisha vijana wa lahaja husika kuishughulikia na kuitumia vizuri lahaja ya eneo husika.
- iii) Watafiti hasa wa lahaja husika waandae tafiti za lahaja hizo kwa kutumia lahaja husika ili kutoa uhalisi wa lahaja yenyewe inavyotumika kwa kuzingatia msamiati wake halisi.
- iv) Waandishi wa vitabu na wanataluma mbalimbali wanajukumu la kuandika kwa lengo la kukunza, kueneza na kuhamasisha matumizi ya lahaja za

Kiswahili. Machapicho hayo yakienea ulimwenguni yanaweza kukuza na kuzipa uhai lahaja za Kiswahili.

- v) Baraza la Kiswahili Zanzibar liandae vipindi maalumu vinavyohusiana na lahaja ya Kimakunduchi. Kama vile maigizo na sanaa za maonyesho ambayo yataleta ari na mwamko kwa watu wa Makunduchi kukizungumza Kimakunduchi popote walipo.
- vi) Vijana wa Kimakunduchi wanatakiwa kuimarisha lahaja popote walipo bila ya kuchelea, kuona
- vii) aibu kwa kuogopa kuonekana washamba au kujisikia watu wa chini kwa kuzungumza lahaja ambayo si maarufu na haifahamiki ipasavyo mbele ya watu wengi.

### **5.3.2 Mapendekezo Kwa Tafiti Zijazo**

Mtafiti anapendekeza kufanywa kwa tafiti zaidi kwenye tanzu mbalimbali zinazohusu lahaja za Kiswahili kikiwemo Kimakunduchi. Tafiti hizo zitazidi kuchimbuwa hazina ya maarifa yaliyofumbatwa kwenye lahaja za Kiswahili. Maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa utafiti ni kuhusu matamshi sahihi ya lahaja kama vile ya Kitumbatu au Kimakunduchi, nafasi ya Kimakunduchi katika kuinyanya lugha ya Kiswahili, sababu zinazosababisha kupotea kwa msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi na athari za michezo ya jadi ya watoto kwa jamii ya sasa na jamii iliyopita. Mapendekezo ya utafiti huu yanatarajiwa kupunguza au kuondoa kabisa mapungufu yaliyopo. Aidha utekelezaji wake utasukuma maendeleo ya lahaja kwa ujumla na kuinua hadhi ya lahaja hizo na Kiswahili kwa jumla.

## MAREJELEO

- Ali, M. M. (2016), Athari za Utandawazi katika Lahaja ya Kitumbatu. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Babbie E. (1999), *The Basic of Social Research*, Belmont: Wads Wourth Publishing Company.
- Bakari (2015), *Ulinganishaji wa kiisimu kati ya lahaja ya Kipemba na Kitumbatu*. Tasnifu ya shahada ya umahiri ya Kiswahili, Chuo kikuu Huria cha Tanzania.
- BAKIZA, (2010), Kamusi la Kiswahili Fasaha. Nairobi: Oxford University Press.
- Barasa, S. & Mous, M. (h.t). *The Oral and Written Interface in SMS: Technologically Mediated Communication in Kenya*. LeidenUniversity.  
<http://www.lotpublications.nl/publish/articles/004164/bookpart.pdf>.
- Imepakuliwa tarehe 03/07/2018.
- Beerkens, (2006), Globalization, <http://www.beekers.inf/file/globalizes.pdf> 200.
- Imepakuliwa tarehe 13/07/2018.
- Brody, N. et.al. (2009), *Its gt 2gthr 18r: Text Messaging as Relational Maintenance Tool*. <http://kycommunication.com/jenniferpdf/Brody.pdf>. Imepakuliwa tarehe 07/09/2018.
- Crystal, D. (2008), *Texting the gr8 db8*. Oxford: Oxford University Press.
- Enon, C. J. (1998), *Education Research and Measurement*. Department of Distance Education; Makerere University. Uganda.
- Geertsema, S. et.al. (2011), Short Message Services (sms) Language and Written Language Skills: Educators' Perspective. *South African Journal of Education*. Volume 31, 475-487.  
<http://www.ajol.info/index.php/sage/article/download/73742/64426>.
- Imepakuliwa tarehe 10/08/2018.

- Khamis, A. A. (2016), Utandawazi katika Utamaduni wa Vijana wa Kizanzibar. JAHAZI, Na. 1, BAKIZA, Zanzibar.
- King'ei, K. na Kobia, J. (2007), Lughha Kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini Kenya. *Nordic Journal of African Studies*. Vol. 16, No. 3, 320–332.
- Kipacha, (2012), *Launi za Kiswahili sanifu na Kiswahili fasaha kwa Tanzania Bara na visiwani Zanzibar* Swahili from 19 (2012) p,1-22.
- Kombo na Tramop D. (2006), Proposal and Thesis Writing Introduction: Nairobi Publisher Publication Africa.
- Kothari, C. R. (2004), Research Methodology; Method and Techniques (toleo la pili) New Delhi New Age International (p) limited Publisher.
- Kress, T. M. (2008), *Critical Praxis Research: Breathing New Life into Research Methods for Teachers*. United States of America: Springer.
- Massamba, D. P. B. (2009), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya lugha*. TUKI, Chuo kikuu cha Dar-esalam.
- Matembai A. (2011), *Kukitandawazosha Kiswahili kupitia simu ya kiganjani, Tafakari kuhusu isimu jamii*, Volume 18:198-210.
- Mbarouk, J. M. (2015), Athari za Sayansi na Teknolojia katika Hadithi za Watoto: Mifano ya Ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba. Tasnifu ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mjawiri, M. M. (2016), Hali ya Kiswahili Zanzibar na Mustakibali Wake. JAHAZI Na. 1, BAKIZA, Zanzibar.
- Angel, L. (2004). Gendered, Bilingual Communication Practices: Mobile Text Messaging Among Hong Kong Collage Students. *Fibre Culture: Mobility, New Social Intensities and the Coordinates of Digital Networks*. Volume 6. <http://www.fibreculture.org/journal/issue6/issue6-lin.html>. Imepakuliwa tarehe 11/08/2018.
- Mohammed, N. A. (2013), Mtazamo wa Wanafunzi na Walimu Kuhusu Matumizi ya Lughha Tandawazi katika Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Mphahlele na Mashamaite K. (2005), The Impact of Shot Message Service (sms) language of ligistic proficiency of lerning and the sms Dictionaries: a challenge for education and Lexsicigraphers. Katika IADS International conference Mobile Learning 161 -168. Imepakuliwa tarehe 10 /08/2018.
- Ong'onda, N. A. et.al. (2011), Syntactic Aspects in Text Messaging. *World Journal of EnglishLanguage*, 1, 2-8. <http://www.sciedu.ca/journal/index.php/wje/>. Imepakuliwa tarehe 09/07/2018.
- Rafi, M. S. (h.t). *SMS Text Analysis: Language, Gender and Current Practices*.<http://www.tesol-france.org/Documents/Colloque07/SMS/>. Imepakuliwa tarehe 09/07/2018.
- Stigand, C. H. (1915), Dialects in Swahili .Cambridge University.
- Walliman, N. (2011). *Reseach Methods: The Basic*. London & New York: Routledge Taylor & Francis Group.
- Wamitila, K. W. (2003), Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia. Focus Books, Nairobi Kenya.
- Whitey W. (1969), Swahili Great Britain. The Rise of National Language low Brydon.

## VIAMBATISHO

### **A: MIONGOZO YA DODOSO, MAHOJIANO NA USHUHUDIAJI**

#### **A 1 MUONGOZO WA DODOSO**

MASWALI YA DODOSO KWA AJILI YA WATAFITIWA WANAOJUA KUSOMA NA KUANDIKA WA MKOA WA KUSINI UNGUJA (MAKUNDUCHI).

**MADA:** Athari ya Mwingiliano wa Kiswahili sanifu Katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi.

Mimi Zubeida Moh'd Chum nnasoma Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Nasoma Kiswahili na nafanya Utafiti juu ya mada isemayo “Athari ya Mwingiliano wa Kiswahili sanifu katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi”.

Tafadhali jaza dodoso hili kwa umakini. Taarifa utakazozitoa ni siri ya mtafiti na mtafitiwa na ukazingatia taarifa hizo zitasaidia na kuendeleza taaluma ya isimu jamii katika Nyanja mbali mbali katika mawanda ya kitaaluma.

**SEHEMU A:** Maelezo binafsi kwa watafitiwa.

Tafadhali jaza nafasi zilizowachwa wazi.

- i) Umri..... ii) Jinsi.....
- ii) Mahala unapoishi.....
- iii) Kiwangochako cha elimu.....

**SEHEMU B:** Maelezo kuhusu mada husika

1. Je kuna tofauti yoyote ya kimaongezi inayojitokeza kati ya wazee na vijana wakati wa mawasiliano yao kupitia Lahaja ya Kimakunduchi?  
Ndio ( ) hapana ( )
2. Katika lahaja ya Kimakunduchi katika hali ya kawaide, wanatumia maneno yafuatayo; tafadhali jaza maneno ambayo wanatumia vijana badala ya maneno hayo.

Maneno ya Kimakunduchi

Maneno ya Vijana wa Makunduchi

- i. Vevi
- ii. Kale

Karibu

iii. Vano

iv. Chuwa

Ongeza maneno ambayo yameathirika kutokana na mwingiliano wa Kiswahili sanifu katika lahaja hiyo

.....

.....

3. Miongoni mwa sababu zinazopelekea uwepo wa tofauti hizo za msamiati katika lahaja ya Kimakunduchi ni:-

i. Mchanganyiko wa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

Kweli ( ) Si kweli ( )

ii. Athari ya Kielimu kwa wanajamii wa Makunduchi  
Kweli ( ) Si kweli ( )

Ongeza sababu nyingine ambazo ni za msingi katika kuathirika kwa lahaja ya Kimakunduchi kimsamiati na kimaana.

.....

.....

4. a) Je kuna msamiati wowote ambao unatumika Makunduchi ambao ni tofauti na msamiati wa Kimakunduchi.

Ndio ( ) hapana ( )

b) Kama ndio orodhesha maneno matano ambayo awali yalitumika vyengine na sasa yanatumika vyengin kwa mfano

Neno la asili

Neno la kisasa

a) baabaa

barabara

b) .....

.....

c) .....

.....

d) .....

.....

e) .....

.....

5. a) Je unafikiri mwingiliano wa Kiswahili sanifu katika Kimakunduchi umesaidia au umedumaza msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi?

umesaidia ( ) umekidumaza ( )

- b) Kama umekidumaza ni maneno gani yaliyoachwa au maneno yaliyoibuka kutokana na maendeleo ya mawasiliano katika jamii ya Makunduchi  
 Maneno yaliyoachwa na kuongezeka

Maneno yaliyoachwa	Maneno yaliyoongezeka
Mfano; Kipanga	Kifuu

6. a) Je unakubaliana na watu wanaosema kuwa matumizi ya TV (runinga), redio, tovuti, fesibuku, na utandawazi kwa ujumla yamechangia kuleta mabadiliko ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi?

Ndio (      ) hapana (      )

- b) Kama ndio taja angalau maneno matano ya Kiswahili sanifu yatokanayo na matumizi ya vyombo tulivyovitaja hapo juu na kutumika katika lahaja ya Kimakunduchi.

Kwa mfano, kimbilia, kataa na kutaka.

- a) .....
- b) .....
- c) .....
- d) .....
- e) .....

7. Kutokana na mabadiliko hayo, nini hatima ya lahaja ya Kimakunduchi kutokana na wimbi kubwa la ukuaji na uenezi wa Kiswahili sanifu?

.....  
 .....  
 .....  
 .....

8. Toa maoni yako kwa jumla kutokana na maendeleo ya mawasiliano katika jamii ya Makunduchi, kuhusiana na athari yake katika msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi



## A 2 MUONGOZO WA MAHOJIANO

### **MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA WATAFITIWA NA WAZUNGUMZAJI WA LAHAJA YA KIMAKUNDUCHI**

**MADA.** Athari ya Mwingiliano wa Kiswahili sanifu Katika Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi.

Maswali

1. Je, wewe ni mtumiaji na mjuzi wa lahaja ya Kimakunduchi?
2. Je, kuna msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi uliobadilika kimaana? Elezea sababu za mabadiliko hayo.
3. Masuala ya redio, TV, simu na suala la kutembelewa na wageni yanafaida gani katika jamii ya Makunduchi; lahaja na utamaduni wake?
4. Masuala hayo hapo juu yamekuza au yamedumaza vipi lahaja ya Kimakunduchi?
5. Kuna maneno gani yaliyoachwa, yaliyoongezeka au yaliyobadilika maana ya maneno ya lahaja ya Kimakunduchi kutokana na maendeleo ya mawasiliano, kama vile kuwepo kwa redio, TV, simu za mkononi na maingiliano ya wageni katika jamii ya Makunduchi?
6. Kuna mustakbali gani wa uwepo wa lahaja ya Kimakunduchi kutokana na athari za mwingiliano wa Kukuaji na ueneaji wa Kiswahili sanifu na utandawazi duniani?
7. Una maoni gani kwa maendeleo ya mawasilano juu ya kukua na kuendelea kwa Kiswahili sanifu na mwingiliano katika lahaja ya Kimakunduchi?

### A 3 MUONGOZO WA USHUHUDIAJI KWA MTAFITI

Dokezo za kufuatwa

- i. Mtafiti atashirikiana na wenyiji (msaidizi mtafiti ) katika kupita maeneo tofauti yanayozungumza Lahaja ya Kimakunduchi
- ii. Mtafiti atashuhudia na kusikiliza mazungumzo ya watumiaji wa lahaja ya Kimakunduchi ili kusikia misamiati na kuweza kugundua kwa kiasi gani msamiati huo umeweza kuimarika au kudhoofika kutokana na utandawazi.
- iii. Mtafiti atasikiliza maneno na kuweza kuchunguza mabadiliko ya maana, maneno ya kale na maneno yaliyoongezeka kutokana na athari ya mwingiliano wa Kiswahili sanifu.
- iv. Mtafiti atachunguza tofauti ya matumizi ya maneno kati ya wazee wa Makunduchi na vijana na kuweza kubaini athari za umwingiliano wa Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi.
- v. Mtafiti atarikodi mazungumzo ya wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi ili kupata matamshi sahihi ya misamiati wa lahaja ya Kimakunduchi ili kurahisisha uchambuzi wa data zake.

**B: RAMANI INAYOONESHA MAENEKO YA UTAFITI**



C: PICHA YA AKINA MAMA WA MAKUNDUCHI WALIOKWENDA  
KUOA MJINI UNGUJA WAKIWA KATIKA SHEREHE ZA HARUSI  
ZILIZOTAWALIWA NA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

